WILLIAM SHAKESPEARE

Mabepari wa Venisi

kimetafsiriwa na

JULIUS K. NYERERE

WILLIAM SHAKESPEARE

MABEPARI WA VENISI

kimetafsiriwa na

JULIUS K. NYERERE

Dar es Salaam
OXFORD UNIVERSITY PRESS
Nairobi

Oxford University Press

OXFORD LONDON GLASGOW
NEW YORK TORONTO MELBOURNE AUCKLAND
NAIROBI DAR ES SALAAM CAPE TOWN
KUALA LUMPUR SINGAPORE HONG KONG TOKYO
DELHI BOMBAY CALCUTTA MADRAS KARACHI

and associated companies in
BEIRUT BERLIN IBADAN MEXICO CITY

ISBN 0 19 572170 5

© Oxford University Press 1969

Reprinted 1970, 1974, 1977, 1981 (twice)

Mchezo huu unalindwa na Sheria ya Haki ya Kunakili na kila ombi la kutolea hadharani (ila kutoka kwa vyuo ambavyo vyote vinaruhusiwa kuutolea bure) lazima lipelekwe kwa Oxford University Press P.O. Box 72532 Nairobi

Sura ya mbele imechorwa na
SEFANIA TUNGINIE

Published by Oxford University Press, East and Central Africa, P.O. Box 5299, Dar es Salaam, Tanzania and printed by English Press, P. O. Box 30127, Accra Road, Nairobi, Kenya.

FAHARISI

Waliomo katika mchezo	vi
Kitendo cha kwanza	
Onyesho la kwanza	1
Onyesho la pili	7
Onyesho la tatu	11
Kitendo cha pili	
Onyesho la kwanza	17
Onyesho, la pili	19
Onyesho la tatu	25
Onyesho la nne	26
Onyesho la tano	27
Onyesho la sita	30
Onyesho la saba	32
Onyesho la nane	35
Onyesho la tisa	37
Kitendo cha tatu	
Onyesho la kwanza	41
Onyesho la pili	45
Onyesho la tatu	56
Onyesho la nne	57
Onyesho la tano	60
Kitendo cha nne	
Onyesho la kwanza	63
Onyesho la pili	77
Kitendo cha tano	
Onyesho la kwanza	79

WALIOMO KATIKA MCHEZO

MTAWALA WA VENISI (*Duke of Venice*)

MWANA WA MFALME WA MOROKO	(*Prince of Morocco*)	Waposi wa Poshia
MWANA WA MFALME WA ARRAGONI	(*Prince of Arragon*)	

ANTONIO (*Antonio*)	Bepari wa Venisi
BASSANIO (*Bassanio*)	Rafiki yake Antonio
GRATIANO (*Gratiano*) SALANIO (*Solanio*) SALARINO (*Salerio*)	Rafiki zake Antonio na Bassanio
LARENZO (*Lorenzo*)	anampenda Jessika
SHAILOKI (*Shylock*)	Yahudi mwenye mali
TUBALI (*Tubal*)	Yahudi, Rafiki yake Shailoki
LAUNSELOTI GOBBO (*Launcelot Gobbo*)	Mchekeshaji, Mtumishi wa Shailoki
MZEE GOBBO (*Old Gobbo*)	Baba yake Launseloti
LEONADO (*Leornado*)	Mtumishi wa Bassanio
BALTAZARI (*Balthazar*) STEFANO (*Stephano*)	Watumishi wa Poshia
POSHIA (*Portia*)	Mrithi tajiri
NERISSA (*Nerissa*)	Mtumishi wa Poshia
JESSIKA (*Jessica*)	Binti yake Shailoki

Mamwinyi wa Venisi, Maofisa wa Mahakama, Mlinzi-Jela, Watumishi wa Poshia, na Watumishi wengine.

I·1

Venisi. Barabarani

(*Aingia Antonio, Salarino na Salanio.*)

ANTONIO: Kusema kweli sijui kisa cha huzuni yangu;
Inanitabisha sana; wasema yakutabisha;
Bali nilivyoipata au kuiambukizwa,
Au imejengekaje, imezawa jinsi gani,
Ningali sijafahamu.
Na huzuni yanifanya kuwa kama punguani,
Kunifanya nisiweze kujifahamu mwenyewe.
SALARINO: Moyowo wasukwasukwa kule juu ya bahari;
Kwenye merikebu zako na matanga yalojaa;
Zipitazo baharini kana kwamba ni mabwana
Na raia matajiri walo juu ya mawimbi,
Au kama maonyesho yapitayo baharini
Yakitazama kwa chini vyombo vidogo vidogo,
Ambavyo havina budi viiname kwa heshima,
Yanapovipita kasi kwa mabawa ya matanga.
SALANIO: Nakwambia kweli, bwana, ningalikuwa na meli
Kama hizo safarini, basi na mapenzi yangu,
Yangekuwa huko huko, ninakotumainia.
Ningaliokota nyasi na kuzitosa hewani,
Ili niweze kujua upepo unavyovuma;
Ningechunguza ramani ili nione bandari,
Forodha na barabara; na kila kinachoweza
Kunitia mashakani juu ya mashua zangu,
Kingenijaza huzuni.
SALARINO: Hata upepo mdogo
Wa kupozea mchuzi, ungalinitia homa,

Kwa kufikiria dhara ya upepo baharini.
Nisingeona mchanga wa saa kutiririka,
Halafu nisiwazie vilindi na maji mafu;
Na kuona chombo changu, chenye kujaa shehena,
Kimekwama mchangani, chashusha matanga yake
Kuzipita mbavu zake yabusu kaburi lake.
Na kama ningalikwenda kanisani na kuona
Jumba takase la mawe, je, nisingefikiria
Miamba yenye hatari, iliyoko baharini,
Ambayo ikivigusa vyombo vyangu viororo,
Itatawanya shehena yake juu ya bahari,
Na kuyavisha mawimbi makali hariri zangu?
Kwa kifupi, vyote hivi, vitu vya thamani kubwa,
Viwe vimeteketea? Nitakuwa na mawazo
Ya kuwaza mambo hayo, na nikakoswa mawazo
Kwamba nikififikwa haya lazima nihuzunike?
Lakini usinambie: nafahamu Antonio
Kinachomhuzunisha hivyo ni bidhaa zake.

ANTONIO: La, sivyo, niamininі: Nashukuru nyota yangu,
Bidhaa zangu haziko katika chombo kimoja,
Au mahali pamoja; wala hali yangu yote,
Si kwamba yategemea bahati ya mwaka huu:
Basi, si bidhaa zangu zinazonihuzunisha.

SALANIO: Kama sivyo ni mapenzi

ANTONIO: Kefule, kefule! Sivyo!

SALARINO: Na wala siyo mapenzi? Tuseme una huzuni,
Sababu huna furaha: na ingekuwa rahisi
Kwako ukirukaruka na kucheka ukisema,
Kwamba unayo furaha kwa kuwa huna huzuni.
Kwa jina lake Janusi alo na vichwa viwili,
Ulimwengu umeumba watu wanaoshangaza:
Wako wanochungulia machoni mwao daima,
Na kucheka kikasuku kwa mpigaji zumari;
Na pia kuna wengine wenye tabia ya siki,

Hawa meno yao kamwe huyaoni kwa kicheko,
Angaapa Nestori kwamba jambo lachekesha.
(*Waingia Bassanio, Lorenzo na Gratiano*)

SALANIO: Huyu Bassanio aja, jamaayo mtukufu,
Gratiano na Lorenzo. Na sasa basi, kwa heri:
Tunakuacha pamoja na wenzi bora zaidi.

SALARINO: Ningependa nikakaa hadi nikuchangamshe,
Kama marafiki bora wasingelinizuia.

ANTONIO: Ninakuthamini sana; tuseme una shughuli,
Na sasa waitumia nafasi hii kwondoka.

SALARINO: Habari za asubuhi, enyi bwana zangu wema.

BASSANIO: Mabwana wema pamoja, tutacheka siku gani?
Semeni! Hamwonekani: Ni lazima uondoke?

SALARINO: Twendea shughuli zetu nanyi mmalize zenu.
(*Salarino na Salanio wanaondoka*)

LORENZO: Bwana wangu Bassanio, umempata Antoni,
Basi sisi tutakwacha: ila saa za jioni,
Tafadhali, fikiria ni wapi tutakutana.

BASSANIO: Sitakosa.

GRATIANO: Haliyo si nzuri sana, Maulana Antonio;
Wajali mno dunia: wote wanaojaribu
Kuinunua kwa taabu, hawaipati dunia:
Niamini, nakwambia, umebadilika mno.

ANTONIO: Kwangu mimi, Gratiano, dunia ni dunia tu,
Na dunia ni jukwaa, juu yake kila mtu
Hucheza sehemu yake. Yangu mimi ni huzuni.

GRATIANO: Yangu na iwe ya juha.
Kwa furaha na vicheko acha makunyanzi yaje,
Afadhali ini langu liungue kwa mvinyo,
Kuliko moyo baridi kwa huzuni ifishayo.
Kwa nini mtu ye yote mwenye damu moto ndani,
Akae kama ni jiwe la sanamu ya babuye?
Alale awapo macho? Awe manjano kwa nyongo
Kwa sababu ya kununa? Nakwambia, Antonio—

Nakupenda, na mapenzi yangu ndiyo yasemayo—
Iko aina ya watu ambao wanazo nyuso
Zilotandwa kwa ukoga kama ni dimbwi tulivu;
Hung'ang'ania ukimya ili eti wadhaniwe
Kuwa ni wenye busara, makini na utulivu;
Kama kwamba wanasema, 'Mimi ni Bwana Busara,
Nitapoanza kusema, kila mtu anyamaze!'
Ee, Antonio wangu, najua baadhi yao
Wenye sifa ya busara kwa kutosema cho chote;
Ingawa nina hakika, kwamba kama wangesema,
Karibu wangelaani masikizio ambayo
Kwa kuwasikia wao yangeta menzi majinga.
Nitakwambia mengine zaidi siku nyingine:
Bali kwa chambo huzuni usijaribu kuloa
Mkizi mjinga sana—sifa ya kuwa mwerevu.
Njoo, Lorenzo mwema. Basi kwa heri kwa sasa:
Nitamaliza nasaha hapo ba'da ya chakula.

LORENZO: Kwa sasa tutakuacha mpaka wakati huo:
Nami pia bila shaka ni mmoja wao hao
Wenye busara mabubu: Kwa sababu Gratiano
Haniachii kusema.

GRATIANO: Ukizidi kuwa nami myaka miwili zaidi
Hutaweza kutambua sauti yako mwenyewe.

ANTONIO: Kwa herini: nitaanza kusema kwa jambo hili.

GRATIANO: Asante sana; maana ukimya unafaa tu
Kwenye ulimi wa ng'ombe ulokwisha kukaushwa.

(*Gratiano na Lorenzo wanaondoka*)

ANTONIO: Hivyo ndiyo wasemaje?

BASSANIO: Gratiano husema zaidi mambo yasiyo na maana, kuliko mtu mwingine ye yote katika Venisi nzima. Hoja zake huwa kama punje mbili za ngano zilizojificha katika pishi thelathini za kumvi: Utatafuta kutwa ndipo uzipate; na utakapozipata hazistahili ile taabu ya kuzitafuta

ANTONIO: Basi, sasa niambie, ni bibie gani yule,

Ambaye ulimwapia hija ya kisirisiri
Na ukaniahidia utaniambia leo?

BASSANIO: Wafahamu, Antonio, nilivyoidhoofisha
Hali na wasaa wangu kwa fahari na makuu
Kuliko uwezo wangu uwezavyo kuhimili:
Na wala sinung'uniki kwa huko kufupishiwa
Maisha ya ubadhiri; bali kinisumbuacho
Ni kutoka kwa heshima kwenye madeni makubwa,
Ambayo wakati wangu, nilipokifuja mali,
Yakawa yameniganda. Kwako wewe, Antonio,
Nimefadhilika mno, kwa fedha na kwa mapenzi;
Na sababu ya mapenzi yako ninayo ruhusa
Kukujulisha mipango na makusudio yangu,
Jinsi ya kuondokana na madeni yangu yote.

ANTONIO: Basi, Bassanio mwema, niambie, tafadhali,
Na kama mipango hiyo, mwenyewe unavyosema,
Ni mipango ya heshima, basi kuwa na hakika,
Ya kwamba nilicho nacho, nafsi yangu mwenyewe,
Na hali na mali yangu, japo ya mwisho kabisa,
Yote imewekwa wazi, kwa mahitajio yako.

BASSANIO: Nilipokuwa shuleni nikipoteza mshale
Nilitupa na wa pili wa namna ile ile,
Niuangalie vema ukienda kule kule
Kupata ulopotea. Kwa kujasiri mwili
Mara nyingi niliweza kupata yote miwili.
Nataja ya utotoni kwa kuwa yafuatayo
Ni ya ujinga mtupu, ya ujinga wa kitoto.
Wewe waniwia mengi, na kama mwana mtundu
Yote nimeyapoteza; walakini ukipenda
Kutupa tena mwingine, uendeko kule kule
Ulikotupa wa kwanza, mimi sinayo mashaka,
Kuangalia shabaha, nipate yote miwili,
Au kukurudishia ule ulotupa nyuma,
Na kwa mshale wa kwanza niwe mdeni daima.

ANTONIO: Unanijua vizuri, na wapoteza wakati
Kusihi mapenzi yangu kwa uwingi wa maneno;
Na kwa sababu ya shaka, kwa kutokuniamini
Kwamba nitakuamini, wanikosea zaidi,
Kuliko kuteketeza mali yote nilo nayo:
Tafadhali niambie, wataka nifanye nini,
Cho chote unachojua kuwa naweza kufanya
Nami nitakitimiza: basi sema, tafadhali.

BASSANIO: Belimonti kuna bibi mwenye urithi mkubwa:
Naye ni mzuri sana kulizidi hilo neno,
Mwenye sifa za ajabu: pengine kwa macho yake
Nimepokea risala zisokuwa na maneno:
Jina lake ni Poshia; hakuna azidiwacho
Na yule bintiye Kato, Poshia wa Burutusi:
Na sifaze huyo bibi zimeenea dunia;
Kwani pepo zote nne zitokazo kila pwani
Huja na waposa bora; na nywele zake kunjufu
Huning'inia pandeni kama sufu ya dhahabu;
Na kufanya Belimonti kuwa kama Kolkosi,
Ambako Jasoni wengi hufika kumtafuta.
Oo, Antonio wangu, ningekuwa na uwezo
Wa kuenda kushindana na mmoja wao hao,
Moyo wanibashiria kuwa ningebahatika!

ANTONIO: Wafahamu mali yangu iko ng'ambo baharini,
Na wala sinayo mali au bidhaa yo yote
Kupata fedha haraka: basi nenda kajaribu
Kupata unachoweza kwa jina langu Venisi:
Nacho kitapatikana kikupatie wasaa
Uendee Belimonti kwake Poshia kizuri
Nenda hima kaulize, nami nitafanya vivyo,
Popote zilipo fedha: nami siulizi swali
Ukipata kwa dhamana au kwa ajili yangu.

(*Wanatoka*)

I·2

Belimonti. Chumba katika nyumba ya Poshia

(*Aingia Poshia na Nerissa*)

POSHIA: Kusema kweli, Nerissa, huu mwili wangu mdogo Umechoshwa na dunia kubwa hii.

NERISSA: Ungechoshwa kweli, bibie mwema, kama maafa yako yangekuwa ni mengi zilivyo baraka zako: Lakini hata hivyo, kama ninavyoona, waelemewao na wingi wa bahati wana taabu vile vile kama wanaokufa na njaa kwa kutokuwa na kitu. Kwa hiyo si furaha ndogo kuwa mtu wa wastani: wingi mno wa mali huharakisha mvi, lakini mali ya kiasi hurefusha maisha.

POSHIA: Hizo ni kanuni bora, na zimetamkwa vema.

NERISSA: Zingalizidi ubora kama zingalifuatwa.

POSHIA: Kama kutenda mema kungekuwa ni rahisi kulivyo kujua mema, vikanisa vingekuwa makanisa, vibanda vya maskini vingekuwa majumba ya kifalme. Ni mbashiri mwema atendaye aonyayo. Naweza zaidi kufundisha watu ishirini ni nini jema la kufanya, kuliko kuwa mmoja wao kufuata mafunzo yangu mwenyewe. Ubongo waweza kuitungia damu sheria; lakini moyo moto huruka sheria baridi: wazimu wa ujana ni sungura ambaye huruka juu ya kiwete shauri jema. Lakini hoja hoja hizi hazitanisaidia kuchagua mume. Ole wangu, neno 'kuchagua!' sina ruhusa kuchagua nimpendaye au kukataa nisiyempenda; na kwa njia hii utashi wa binti hai umekinzwa na wasia wa baba marehemu. Je, si taabu, Nerissa, kwamba siwezi kuchagua wala kukataa ye yote?

NERISSA: Baba yako alikuwa ni mwadilifu daima: na watu watakatifu wakati wa kufa hupata maongozi mema: kwa hiyo, bahati nasibu hii aliyobuni katika masanduku

matatu haya, la dhahabu, la fedha na la risasi—ambayo kwayo atakayechagua utashi wake atakuwa kakuchagua wewe—bila shaka haitachaguliwa vema na mtu asiye kupenda hasa. Lakini unampenda nani kati ya waposaji hawa wana wa kifalme ambao wamesha kuja?

POSHIA: Nakusihi, wataje; na utakavyowataja nitawaeleza; na kutokana na maelezo yangu bahatisha mapenzi yangu.

NERISSA: Kwanza, yuko mwana wa mfalme wa Neapoli.

POSHIA: Naam, yeye hasa ni mwana farasi; kwani hana maongezi mengine ila juu ya farasi wake; na hufanya kuwa ni nyongeza ya sifa zake kwamba yeye mwenyewe anaweza kumvisha chuma miguuni.

NERISSA: Halafu kuna Kaunti wa Palatine.

POSHIA: Yeye hana afanyalo ila kukunja uso; kama anayesema: 'Na ikiwa hunitaki, chagua': husikia hadithi nzuri, hacheki: sina shaka atakapokuwa mzee atakuwa filosofa mliaji; kwani katika ujana wake ana huzuni nyingi mno isiyo na adabu. Afadhali niolewe na kichwa cha mauti chenye mfupa kinywani kuliko kuolewa na ye yote kati yao. Mungu aniepushe na wawili hao!

NERISSA: Wasemaje juu ya maulana Mfaransa, Bwana Le Bon?

POSHIA: Mungu alimuumba na kwa hiyo naakubaliwe kwamba ni mtu. Kwa kweli, najua ni dhambi kudhihaki; lakini, yeye! Lo, anasema zaidi juu ya farasi wake kuzidi yule Mneapoli; ana tabia mbaya zaidi ya kukunja uso kuliko ile ya Kaunti wa Palatine; yeye ni kila mtu katika tufe la mtu; kama ndege akiimba mara ataanza kuchachawa; hupigana kwa panga na kivuli chake mwenyewe; nikiolewa naye nitakuwa nimeolewa na waume ishirini. Akinipuuza, nitamsamehe; kwani akinipenda kama mwenda wazimu, kamwe sitaweza kumlipa mapenzi yake.

NERISSA: Wasemaje, basi juu ya Falikani Kivuko, yule kijana kabaila wa Kiingereza?

POSHIA: Unajua, simwambii cho chote, kwani hanielewi, wala mimi simwelewi; hajui Kilatini, Kifaransa, wala Kitaliani; na Kiingereza changu hakina thamani japo ya senti moja. Ana sura nzuri ya mwanamume; lakini, ole wangu, nani aweza kuzungumza na uzuri—bubu? Nguo zake ni shaghala baghala. Nadhani koti lake alilinunua kutoka Italia, stokingi zake kutoka Ufaransa, kofia yake kutoka Ujerumani, na tabia yake kutoka kila mahali.

NERISSA: Na wamwonaje jirani yake, Maulana wa Kiskochi?

POSHIA: Ana mapenzi ya kijirani; kwani aliazimwa kofi na mwenziye na wala asimrudishie. Alisema atamlipa baadaye atakapoweza: nadhani Mfaransa ndiye aliyekuwa mdhamini wake, aliyeahidi kwamba siku moja kofi hilo litalipwa.

NERISSA: Na kijana Jerumani wampendaje, yule mpwa Wa Sultani wa Saksoni?

POSHIA: Mbaya sana asubuhi, anapokuwa hajalewa; na mbaya zaidi adhuhuri anapokuwa kesha kulewa: anapokuwa na hali nzuri kabisa huwa bado ni chini ya utu, na anapokuwa mbaya kabisa huwa anamzidi mnyama. Nanipatwe na mkosi wo wote mbaya, lakini nisiolewe naye.

NERISSA: Kama na yeye atakubali kuchagua, na akachagua sanduku lenyewe, utakuwa hukutimiza wasia wa baba yako, ikiwa utamkataa.

POSHIA: Kwa ajili hiyo, kwa kuogopa ovu kama hilo lisije likatokea, nakusihi tafadhali, uweke bilauri kubwa ya mvinyo wa Rhine juu ya sanduku lisilo; kwani japo shetani angalikuwa ndani na kishawishi hicho kiwe nje najua kitamvuta. Nitafanya jambo lolote, Nerissa, niepuke kuolewa na dodoki.

NERISSA: Usihofu, bibie, eti huenda ukaolewa na ye yote kati ya mabwana hawa: wameninong'oneza makusudio yao; ambayo, kwa kweli, ni kurudi makwao, na kuacha

kukubughudhi na posa zaidi, au labda akupate mtu kinyume cha nia ya baba yako, kufuatana na masanduku haya.

POSHIA: Hata ningaliishi mpaka niwe mzee kama Sibilla, nitakufa mwali kama Diana, nisipoolewa kwa jinsi baba alivyousia. Nafurahi kwamba kundi hili la waposaji lina akili; kwani hakuna hata mmoja wao nisiyemtakia kwa heri; na kumwomba Mungu abariki kuondoka kwao.

NERISSA: Hukumbuki, bibie, kabla baba yako hajafa, Mvenisi mmoja, mwanachuoni tena askari, ambaye alikuja hapa pamoja na Mwinyi Mkuu wa Montiferrati.

POSHIA: Naam, naam, alikuwa Bassanio, nadhani ndivyo alivyoitwa.

NERISSA: Ndivyo, bibie; naye, miongoni mwa wanaume wote ambao macho yangu ya kipumbavu yaliopata kuona, ndiye anayestahili kuzidi wote, kumpata bibie mzuri.

POSHIA: Namkumbuka vema; na pia nakumbuka kuwa anastahili sifa yako.

(*Aingia Mtumishi*)

Hali gani! Kuna nini?

MTUMISHI: Wale wageni wanne wanakutaka bibie, wakuage: na kuna mjumbe wa mgeni wa tano, Mwana wa Mfalme wa Moroko, kaleta habari kwamba bwana wake, huyo mwana wa Mfalme, atafika hapa leo jioni.

POSHIA: Ningeweza kumpokea huyo wa tano kwa moyo wa furaha kama ninavyoweza kuwaaga wale wengine wanne ningekufurahia sana kufika kwake: kama ana hali ya malaika au sura ya shetani, ni heri anighofiri makosa kuliko kuniposa. Njoo, Nerissa, wewe, tangulia—Tukimfungia mlango mposaji mmoja, mara mwingine anapiga hodi.

(*Wanatoka*)

Kitendo cha Kwanza: Onyesho la Tatu

I · 3

Venisi. Mahali pa hadhara

(*Aingia Bassanio na Shailoki*)

SHAILOKI: Dukati elfu tatu,—vema.

BASSANIO: Naam, bwana, kwa miezi mitatu.

SHAILOKI: Kwa miezi mitatu, —vema.

BASSANIO: Naam, na kama nilivyokwambia, Antonio Atakuwa mdhamini.

SHAILOKI: Antonio atakuwa mdhamini,—vema.

BASSANIO: Utaweza kunisaidia? Utanifurahisha? Naweza kupata jibu lako?

SHAILOKI: Dukati elfu tatu, kwa miezi mitatu, na Antonio atakuwa mdhamini.

BASSANIO: Jibu lako ni nini?

SHAILOKI: Antonio ni mtu mwema.

BASSANIO: Umepata kusikia jambo lo lote la kinyume juu yake?

SHAILOKI: O, la, la, la, la; maana yangu ya kusema kuwa ni mtu mwema ni kutaka wewe uelewe kuwa anatosha. Lakini uwezo wake ni wa udhanifu: ana merikebu moja iliyokwenda Tripoli, na nyingine Visiwa vya Magharibi. Nasikia pia kutoka katika Rialito ana merikebu ya tatu inayokwenda Mexico, ya nne Uingereza, na anazo shughuli nyingine zilizotapakaa ng'ambo. Lakini meli ni mabao tu, na mabaharia ni watu tu: kuna panya wa nchi kavu na panya wa majini, wezi wa majini na wezi wa nchi kavu—nasema maharamia wa baharini: na halafu kuna hatari ya maji, pepo na miamba. Lakini hata hivyo, mtu huyu anatosha. Dukati elfu tatu; nadhani naweza kukubali dhamana yake.

BASSANIO: Bila shaka utaipata.

SHAILOKI: Bila shaka nitaipata; na ili niwe na hakika nitatafakari.
Naweza kusema na Antonio?

BASSANIO: Ukipenda kula nasi leo jioni.

SHAILOKI: Naam, nikanuse nyama ya nguruwe; nikale katika kundi ambamo nabii wenu Mnazareti alimomfukuzia shetani. Nitanunua nanyi, nitauza nanyi, nitazungumza nanyi, nitatembea nanyi, na kadhalika; lakini kamwe sitakula nanyi, kunywa nanyi au kusali nanyi. Kuna habari gani kwenye Rialito? Nani huyu anayekuja?

(*Aingia Antonio*)

BASSANIO: Ni Bwana Antonio.

SHAILOKI: (*Kando*) Jinsi anavyofanana mtoza ushuru mbembe.
Namchukia kwa kuwa yeye ni Mmasihiya;
Namchukia zaidi sababu ni mpumbavu,
Hukopesha fedha bure, kwa hiyo hutelemsha
Kima cha riba Venisi.
Ningalipata nafasi ya kuweza kumwangusha,
Ningaliiwasha moto husuda nimwoneayo.
Analichukia sana taifa letu teule.
Haachi kunishutumu, hata kunako makundi
Ya wafanya biashara. Anishutumu nafsi,
Pia ununuzi wangu, hata faida ya haki,
Ambayo yeye mwenyewe husema kuwa ni riba.
Na lilaniwe taifa langu, nikimsamehe!

BASSANIO: Shailoki, wasikia?

SHAILOKI: Ningali ninajihoji kwa mali yangu ya sasa;
Na kadiri niwezavyo kukisia nafikiri
Siwezi kupata mara dukati elfu tatu.
Hiyo si kitu. Tubali, Mweburania tajiri,
Mtu wa kabila langu, aweza kunipatia.
Lakini hebu tulia! Wataka myezi mingapi?

(*Kwa Antonio*)

Hali gani, bwana mwema? Ni punde tumekutaja.
ANTONIO: Shailoki, japokuwa sikopeshi, na sikopi,
Kwa kupokea cho chote au kutoa cho chote,
Kinachozidi kiasi, bali kwa kutimiliza
Mahitaji ya rafiki, nitavunja mazoea
(*Kwa Bassanio*) Je, kesha kukuambia kiasi atachoweza?
SHAILOKI: Naam, naam, chote;—dukati elfu tatu.
ANTONIO: Na kwa miezi mitatu?
SHAILOKI: Nilisahau; miezi mitatu; ulivyosema.
Na sasa dhamana yako; hebu, lakini sikia;
Nikidhani ulisema, hukopeshi na hukopi
Kwa ajili ya faida.
ANTONIO: Sina mazoea hayo.
SHAILOKI: Yakobo alipokuwa akiwachunga kondoo
Wa Labani, mjombaye, alikuwa ni wa tatu
Toka kwa Iburahimu wa kwetu mtakatifu,
(Mamaye mwenye busara alivyomfanyizia)
Naam, Yakobo yeye, katika wenye kurithi,
Alikuwa ni wa tatu.
ANTONIO: Sasa ndiyo kusemaje? Kwamba alitwaa riba?
SHAILOKI: La, la, hakutwaa riba; la, jinsi unavyosema,
Si riba ya waziwazi; kumbuka alivyofanya,
Yeye na mjomba wake, Labani, walipatana,
Kwamba wana wa kondoo wote wataozaliwa
Na milia na madoa watakuwa wa Yakobo.
Ilikuwa ni mapito ya kupata, akapata:
Na mapato ni baraka kama siyo ya kuiba.
ANTONIO: Bahati hii Yakobo aliifanyia kazi;
Kitu ambacho hakikuwa kwenye uwezo wake,
Bali kilichofanyizwa kwa mkono wa mbinguni
Je, haya yameingizwa kufanya riba halali?
Dhahabu na fedha zako ni kondoo wanozaa?
SHAILOKI: Hayo mimi sifahamu: lakini nazizalisha
Kwa haraka vile vile: ila nisikie, bwana.

ANTONIO: Sikiliza, Bassanio: Shetani pia aweza,
Kutumia msahafu kujifalia mwenyewe.
Roho ovu iletapo shahidi mtakatifu,
Ni sawa kama haini mwenye uso wa kicheko;
Ni tunda zuri kwa nje, na kwa ndani limeoza;
O, wongo upendezavyo ukitazamwa kwa nje!
SHAILOKI: Dukati elfu tatu; ni hesabu nzuri sana.
Na kwa miezi mitatu, kutoka kwa thenashara;
Hebu, tuone kiasi—
ANTONIO: Sema, basi Shailoki, tutakuwa wadeniwo?
SHAILOKI: Bwana Antonio, mara kwa mara na mara nyingi,
Kule kwenye Rialito kanikemeakemea
Sababu ya fedha zangu na faida nipatayo:
Bali nimevumilia na kupuza kwa subira,
Kwani uvumilivu ni ada ya kabila letu:
Unaniita kafiri, jibwa bazazi, katili,
Na waitemea mate kanzu yangu ya Yahudi,
Na kwa matumizi yote ya kile kilicho changu:
Na sasa yaelekea wanitaka muawana:
Ebo, potelea mbali! Mwaja kwangu na kusema,
Shailoki, twahitaji fedha zako: hivyo hivyo;
Nyie mlonitemea mate kwenye ndevu zangu,
Na kunipiga mateke mpigavyo jibwa geni
Livukapo kizingiti: mnachotaka ni fedha.
Niwaambieni nini? Nisingelisema kwenu,
'Mbwa naye ana fedha? Kweli inawezekana
Mbwa naye akopeshe dukati elfu tatu?'
Au niiname sana na kwa ada ya kitwana,
Huku nikihemahema, kwa unyonge nikisema,
'Bwana, ulinitemea Jumatano ilopita;
Ulinipiga mateke siku fulani fulani;
Na tena siku nyingine ulinitukana mbwa;
Kwa heshima yote hii wewe ulonifanyia,

Nitakukopesha kima kadha wa kadha cha fedha.'
ANTONIO: Naweza nikakuita jina hilo hilo tena,
Nikakutemea mate, na kukudharau pia.
Ikiwa utakopesha fedha hizi, zikopeshe
Si kwa marafiki zako—ni tangu lini rafiki
Alizalisha faida fedha ngumba za rafiki—
Walakini zikopeshe kama kwa adui yako;
Ambaye asipolipa waweza ukamwadhibu
Pasipo kusitasita.
SHAILOKI: Tazama unavyofoka!
Ningependa urafiki nilipate pendo lako,
Na kusahau aibu ambazo umenipaka,
Kisha nikutimizie mahitajio ya sasa,
Bila kuchukua japo senti moja ya faida
Kwa fedha yangu mwenyewe, lakini hunisikii;
Ni wema ninaokupa.
BASSANIO: Huo ungekuwa wema.
SHAILOKI: Nitaonya wema huu: tufatane kwa mwandishi.
Tuwekeane shahada; na kwa jinsi ya furaha,
Ukishindwa kunilipa kwa siku kadha wa kadha,
Pahala kadha wa kadha, kiasi kadha wa kadha,
Kilotajwa na shahada, malipo yake na yawe
Ratili iliyo sawa ya mwili wako mzuri,
Ikatwe po pote pale mimi nitapochagua.
ANTONIO: Niko radhi, kwa imani: nitakubali shahada,
Na kusema kuna wema mwingi kwa Yahudi huyu.
BASSANIO: Usikubali shahada hiyo kwa ajili yangu,
Afadhali nibakie nao uhitaji wangu.
ANTONIO: Ona, Usihofu kitu; sitashindwa kutimiza:
Mnamo myezi miwili, yaani mwezi kabla
Shahada haijatimu, natazamia kurudi
Kwa thamani tatu mara tatu ya shahada hii.
SHAILOKI: O baba Aburahamu, tazama jinsi walivyo,
Watu Masihiya hawa; maovu yao wenyewe

Yawafunza kuyashuku mawazo ya wengineo.
Tafadhali, niambie, ataposhindwa kulipa,
Nitapata tija gani kwa kutoza malipizi?
Ratili moja ya nyama iliyokatwa kwa mtu
Siyo kitu cha thamani, wala siyo cha faida
Kama nyama ya kondoo, au ng'ombe au mbuzi.
Kwa kumtaka hisani namwonyesha urafiki,
Akiupokea, vema; la, hautaki, kwa heri.
Nami, kwa mapenzi yangu, naomba msinidhuru.

ANTONIO: Ndiyo, Shailoki, nitakubali shahada hii.

SHAILOKI: Basi twende tukutane mara moja kwa mwandishi;
Na kumpa maagizo kwa shahada safi hii;
Nami nitakwenda hima kuleta hizo dukati;
Na kuona nyumba yangu niloacha ikilindwa
Na mlinzi hohe hahe, kisha nitarudi hima.

ANTONIO: Haya, enenda haraka, ewe Yahudi mpole.

(*Shailoki anaondoka*)

Yahudi atabatizwa: anaanza kuwa mwema.

BASSANIO: Sipendi maneno mema na mawazo ya maovu.

ANTONIO: Twende zetu: jambo hili halina cha kuhofisha;
Meli zangu zinarudi mwezi mmoja mzima,
Kabla ya siku hiyo.

(*Wanatoka*)

II . 1

Belimonti. Chumba, nyumbani kwa Poshia

(*Sauti ya tarumbeta. Aingia Mwana wa Mfalme wa Moroko na Wafuasi wake; Poshia, Nerissa na baadhi ya watumishi wake*)

MOROKO: Usikose kunipenda kwa sura yangu nyeusi
Niliyovishwa na joto la jirani yangu, jua.
Walakini niletee kiumbe mweupe sana,
Alozaliwa shemali, kule moto wa Fibusi
Usikoweza yeyusha japo shungi la barafu,
Tukatane kwa penzilo, tuone damu ya nani,
Ni yake au ni yangu, ilo nyekundu zaidi,
Nakwambia, bibi, hii sura yangu nyingineyo
Imetisha mashujaa: naapa kwa penzi langu,
Kwamba wanawali bora wa nchi yangu mwenyewe
Na pia wameipenda: sibadili sura hii,
Ila kwa kuibadili niyapate mapenzio,
Malkia wangu mwema.

POSHIA: Kwa kufanya uchaguzi sitaelekezwa tu
Na upekuzi wa macho ya kijana mwanamwali;
Tena, bahati nasibu ya maisha nilopewa
Hainachii ruhusa kuchagua nipendavyo:
Lakini ingalikuwa babangu hakunihini
Kwa hiyo busara yake na kufanya sina budi
Nikubali kuwa mke wa mwanamume ye yote
Atoweza kunipata kwa njia nilokwambia,
Wewe, mtukufu Mwana wa Mfalme, ungekuwa
Na uwezo ule ule wa kupata pendo langu
Kama mgeni ye yote niliyekwisha kumwona.

MOROKO: Hata kwa kauli hiyo nakushukuru, bibie:
Hivyo basi, tafadhali, kanionye masanduku,
Nikajaribu bahati: kwa jambia langu hili,
Lilomwua Sultani wa Uajemi na mwana,
Lilovishinda vita vya Sultani Solimani,
Nitakaza macho yangu kuzidi yote makali,
Nitazidi ujasiri moyo jasiri kwa kwanza,
Nitamnyang'anya dubu watoto wanaonyonya,
Naam, na kumkejeli simba akiunguruma,
Kukupata wewe, bibi. Bali, ole wangu sasa!
Herikule na Lichasi wangeliicheza kamari
Kujua yupi ni bòra, yawezekana mnyonge
Kwa bahati tu nasibu angejaliwa kushinda.
Ndiyo ma'na Alikide kushindwa na boi wake;
Na mimi kwa kuongozwa naye kipofu Bahati
Naweza nikakikosa ambacho aliye duni
Aweza akakipata nami nife kwa majuto.
POSHIA: Huna budi uchague: ama usibahatishe,
Au ukibahatisha utangulie kuapa
Kwamba usipofaulu hutazungumza kamwe
Na mwanamke ye yote kwa kusudi la kuoa:
Basi, fikiri vizuri.
MOROKO: Sina haja kufikiri.
Haya twende, nipeleke bahati yangu iliko.
POSHIA: Kwanza twende hekaluni: na baada ya chakula
Utajaribu bahati.
MOROKO: Na iwe bahati njema! Inifanye mteule,
Myongoni mwa wanaume, au niwe maleuni.
(*Tarumbeta. Wanatoka*)

II . 2

Venisi. Barabarani

(*Aingia Launseloti*)

LAUNSELOTI: Bila shaka siku moja dhamira yangu haina budi inishauri kumkimbia huyu Yahudi bwana wangu. Ibilisi hanachii, bali azidi kunishawishi, akisema, 'Gobbo, Launseloti Gobbo, Launseloti mwema,' na 'Gobbo mwema,' au 'Launseloti Gobbo mwema, tumia miguu yako, toroka, kimbia.' Dhamira yangu yasema, 'La; angalia, Launseloti mwaminifu; angalia Gobbo mwaminifu,' au kama mwanzo, 'Launseloti Gobbo mwaminifu; usikimbie; lipige teke wazo la kukimbia.' Ibilisi jasiri kupita wote anambia nijiendee: 'Shika njia!' anasema ibilisi; 'kimbia!' anasema ibilisi; 'kwa jina la mbingu,' anasema ibilisi, 'piga moyo konde, ukimbie.' Lakini dhamira yangu ambayo imelemea shingo la moyo wangu, inanambia kwa busara sana, 'Rafiki yangu mwaminifu Launseloti, kwa sababu u mwana wa baba mwaminifu au tuseme, u mwana wa mwanamke mwaninifu; - basi, dhamira yangu inasema, 'Launseloti usiondoke kamwe.' 'Ondoka,' asema ibilisi. 'Usiondoke' yasema dhamira yangu. Dhamira, mimi nasema, unanishauri vema; ibilisi, mimi nasema, unanishauri vema: ili nitawaliwe na dhamira yangu itanibidi niendelee kukaa na Yahudi bwana wangu,—ambaye—ashakumu—ni aina ya shetani; nakwambia Yahudi nitakuwa nimetawaliwa na ibilisi ambaye—ashakumu—ndiye shetani mwenyewe. Ni dhahiri Yahudi huyu ni shetani-mtu; na, kwa dhamira yangu, dhamira yangu ni aina ya dhamira ngumu, kuweza kunishauri niendelee kukaa na Yahudi. Ibilisi ananipa shauri la kirafiki zaidi: nitakimbia, ibilisi; miguu yangu iko chini ya amri yako. Nitakimbia.

(*Aingia Mzee Gobbo, ana kikapu*)

GOBBO: Bwana mdogo, wewe, tafadhali, wapi kwa bwana Yahudi?

LAUNSELOTI: (*Kando*) Lo, mbingu, huyu ndiye baba yangu mzazi hasa ambaye kwa sababu ni kipofu kabisa hanitambui: nitajaribu kumbabaisha.

GOBBO: Muungwana Bwana mdogo, tafadhali, ni wapi njia ya kwenda kwa Bwana Yahudi?

LAUNSELOTI: Nenda upande wa kulia penye kona ya kwanza. Lakini, katika kona nyingine ya zote, nenda kushoto; naam, katika kona ifuatayo, usiende kokote, bali nenda chini utafika nyumbani kwa Yahudi.

GOBBO: Kwa watakatifu wa Mungu wote, itakuwa njia ngumu kupata. Waweza kunifahamisha kama mtu mmoja aitwaye Launseloti ambaye anakaa kwake, bado anakaa kwake au la?

LAUNSELOTI: Wauliza juu ya Bwana mdogo Launseloti? (*Kando*) Nisikie sasa; sasa ndiyo nitakoroga maji. Wauliza juu ya Bwana mdogo Launseloti?

GOBBO: Siyo Bwana mdogo, Bwana, bali mtoto wa maskini: baba yake, ingawa naisema mimi, ni mwaminifu kuzidi mtu maskini, na, Mungu ashukuriwe, hali yake haijambo.

LAUNSELOTI: Hali ya baba yake na iweje, twazungumza juu ya Bwana mdogo Launseloti.

GOBBO: Rafiki yako, mheshimiwa, Launseloti tu, Bwana.

LAUNSELOTI: Lakini, tafadhali, kwa hiyo, mzee, kwa hiyo, Nakusihi, wasema Bwana mdogo Launseloti?

GOBBO: Juu ya Launseloti, ukipenda, mheshimiwa.

LAUNSELOTI: Kwa hiyo Bwana mdogo Launseloti. Usiseme juu ya Bwana mdogo Launseloti, baba; kwani kijana mwungwana huyo, kwa kufuata Nujumu na Katiba na usemi mwingine wa ovyo, Dada Watatu, na aina nyingine za elimu, kwa kweli kesha kufariki

dunia; au, kama ambavyo ungesema kwa lugha ya wazi, kesha kwenda mbinguni.

GOBBO: Lo, Mungu apishe mbali, mtoto huyu alikuwa ndiye mkongojo wa uzee wangu, naam, nguzo yangu hasa.

LAUNSELOTI: (*Kando*) Mimi nafanana na gongo, au mhimili banda, au mkongojo au nguzo? Unanifahamu, baba?

GOBBO: Ole wangu, sikujui mwungwana kijana! lakini, tafadhali, nambie, mwanangu, — Mungu abariki roho yake! — yu hai au kafariki?

LAUNSELOTI: Hunijui, baba?

GOBBO: Ole wangu! bwana: mimi ni kipofu kabisa; sikujui.

LAUNSELOTI: La, kwa kweli, hata kama macho yako yangekuwa mazima, ungeshindwa kunijua: ni baba mwenye busara amjuaye mwanae. Basi, mzee nitakwambia habari za mwanao: Kwanza nipe baraka zako (*apiga magoti*): ukweli utadhihirika; mauaji hayawezi kufichika kwa muda mrefu,—mwana wa mtu aweza; lakini hatimaye ukweli utajitokeza.

GOBBO: Tafadhali, bwana, simama: nina hakika wewe siyo Launseloti, kijana wangu.

LAUNSELOTI: Tafadhali, na tuache dhihaka, nipe baraka yako: Mimi ni Launseloti, aliyekuwa kijana wako, aliye mwanao, atakayekuwa mtoto wako.

GOBBO: Siwezi kufikiri kuwa wewe ni mwanangu.

LAUNSELOTI: Sijui kauli hiyo nitaifikiriaje: lakini mimi ni Launseloti, mtumishi wa Yahudi; nina hakika kuwa Margeri mkeo ndiye mama yangu.

GOBBO: Ni kweli jina lake ni Margeri; nitaapa kama wewe ni Launseloti kweli na mwanangu kabisa. Aabudiwe Mungu! Lo, ndevu gani hizi ulizo nazo! Una nywele nyingi zaidi kidevuni kuliko Dobbini farasi wangu alizo nazo mkiani.

LAUNSELOTI: (*Akisimama*) Basi yaelekea kuwa mkia wa Dobbini unakua kwa kurudi nyuma; nina hakika kuwa alikuwa na manyoya mengi zaidi mkiani nilipomwona mara ya mwisho.

GOBBO: Mungu, umebadilika sana! Mnasikilizanaje na bwana wako? Nimemletea zawadi. Unakubali?

LAUNSELOTI: Sema! lakini kwa upande wangu, kwa kuwa nimeamua kukimbia, basi sipumziki mpaka niwe mbali kidogo. Bwana wangu ni Yahudi kweli kweli; umpe zawadi! mpe kitanzi: nakufa na njaa kazini kwake; vidole vyangu vyote unaweza kuvihesabu kwa mbavu zangu. Baba, nafurahi umekuja: nipe zawadi yako nimpelekee bwana mmoja Bassanio, ambaye kwa kweli hutoa mavazi ya tunu: nisipoweza kumtumikia nitakimbilia mbali kadiri ya kiasi cha ardhi ya Mungu. O, bahati tunu! naye ni huyu aja: mpe, baba; kwani mimi ni Yahudi kama nitaendelea kumtumikia Yahudi.

(*Aingia Bassanio na Leonado na baadhi ya wafuasi*)

BASSANIO: Unaweza; lakini fanya haraka ili chakula kisichelewe kupita saa kumi na moja. Peleka barua hizi; agiza mavazi yashonwe; na mwambie Gratiano aje kwangu haraka.

(*Mtumishi anaondoka*)

LAUNSELOTI: Mpe, baba.

GOBBO: Mungu akubariki mheshimiwa!

BASSANIO: Marahaba: ungependa kusema lolote nami?

GOBBO: Huyu mwanangu bwana, kijana maskini,—

LAUNSELOTI: Siyo kijana maskini, bwana, bali mtu wa Yahudi yule tajiri; ambaye angependa, bwana, kama baba atakavyofafanua,—

GOBBO: Ana shauku kubwa, bwana, aweza mtu kusema, kutumikia,—

LAUNSELOTI: Kwa kweli kifupi chake ni kuwa namtumikia Yahudi, na ninayo shauku, kama baba atakavyofafanua,—

GOBBO: Bwana wake na yeye, nisamehe bwana, hawasikilizani sana

LAUNSELOTI: Kwa kifupi, ukweli wenyewe ni kuwa, yule Yahudi; baada ya kunidhulumu, anazidi tena kunifanya, kama baba yangu ambaye, natumaini, kwa kuwa ni mzee atakutobolea vizuri—

GOBBO: Hapa bwana, nina kiasi cha njiwa, ambacho ningependa kukupa mheshimiwa; na ombi langu ni kuwa,—

LAUNSELOTI: Kwa kifupi sana ombi lenyewe linanihusu mimi, kama mheshimiwa utakavyofahamishwa na mzee huyu mwaminifu; na, ingawa naisema mimi, japo mzee, lakini maskini, baba yangu.

BASSANIO: Mmoja awasemee wote..Mwataka nini?

LAUNSELOTI: Kukutumikia, bwana.

GOBBO: Hiyo hasa ndiyo habari yenyewe, bwana.

BASSANIO: Nakufahamu vizuri; umepata ombi lako:
Shailoki bwana wako tumezungumza leo,
Naye amekusifia—ikiwa wapendelea
Kuondoka kwa Yahudi tajiri na kuja kuwa
Mfuasi wa mwungwana maskini kama mimi.

LAUNSELOTI: Methali ya kale imegawanywa vizuri sana kati ya bwana wangu Shailoki na wewe, bwana. Wewe una neema ya Mungu, bwana, na yeye ana mali.

BASSANIO: Umeisema vizuri. Nenda, baba, na mwanao,
Kamuage bwana wako wa zamani, na halafu
Tafuta nyumbani kwangu.—(*kwa wafuasi wake*)
na nyinyi mpeni vazi
Lililopambwa kuzidi la wenzie: timizeni.

LAUNSELOTI: Baba, ndani. Siwezi kupata kazi, la; sina ulimi kichwani mwangu. Vema (*atazama mkono wake*) Kama mtu ye yote katika Italia ana mkono mzuri zaidi, ambaye atakuwa tayari kuapa kwenye kitabu, basi nitapata bahati nzuri! Tazama, huu mstari mzuri wa maisha! huu mkorogo wa wanawake! ole wangu, wake kumi na

mmoja na wanawali tisa ni pato dogo kwa mtu mmoja; na halafu ili kuepuka kufa maji mara tatu na kuponya maisha yangu kwa chupuchupu haya makimbilio hafifu! Vema, kama Bahati ni mwanamke, angalau safari hii kawa mwanamke mwema.—Baba, njoo; kufumba na kufumbua nitamuaga Yahudi.

(*Launseloti na Mzee Gobbo wanatoka*)

BASSANIO: Nakuomba, Leonado mwema, fikiria hili:
Vikisha kununuliwa hivi na kuwekwa vema,
Rudi kwa haraka kwani leo namkaribisha
Sahibu yangu mpenzi: haya, enenda haraka.

LEONADO: Nitafanya niwezavyo.

(*Aingia Gratiano*)

GRATIANO: Bwana wako yuko wapi?

LEONADO: Yule, bwana, atembea. (*Anatoka*)

GRATIANO: Bwana Bassanio!

BASSANIO: Gratiano!

GRATIANO: Nina ombi kwako.

BASSANIO: Umekwisha kulipata.

GRATIANO: Usininyime: lazima tufatane Belimonti.

BASSANIO: Vema, itakuwa. Lakini sikia, Gratiano:
U mshamba, na fidhuli, na mropokaji mno;
Sifa zinokushamiri vizuri na vya kutosha,
Na ambazo kwetu sisi hatuoni ni dosari;
Walakini ugenini zitakuwa si adabu.
Nakuomba tafadhali, jitahidi kupooza
Harara ya moyo wako kwa vijitone baridi
Vya stara na adabu; ama sivyo kutokana
Na tabiayo ya shamba nishindwe kueleweka
Ugenini niendako nikose mradi wangu.

GRATIANO: Ewe Bwana Bassanio, nisikie, tafadhali:
Kama nisipoonyesha tabia ya utulivu,
Na kusema kwa heshima, na kutukana kwa shida;
Na vitabu vya ibada ikiwa sitavibeba,

Nisipokuwa mpole; la, na zaidi ya yote
Neema inaposema, yafunike macho yangu
Hivi kwa kofia yangu, pumua, sema amina;
Kama nisipotimiza kawaida ya heshima,
Kama alosoma vema tabia ya utulivu,
Kumpendeza bibiye—usiniamini tena.

BASSANIO: Vema, tutakutazama.

GRATIANO: Lakini siyo kwa leo: basi msinihukumu
Kwa nitayofanya leo.

BASSANIO: La, ingelihuzunisha:
Kwa sababu ningependa leo uchekeshe sana,
Kwani tuna marafiki wapendao kufurahi.
Walakini kwa herini: nina shughuli nyingine.

GRATIANO: Nami napaswa niende kwa Lorenzo na wengine:
Walakini tutakuja saa za kula jioni.

(*Wanatoka*)

II · 3

Venisi bado. Chumba, nyumbani kwa Shailoki

(*Aingia Jessika na Launseloti*)

JESSIKA: Nasikitika ya kuwa utamwacha baba yangu:
Nyumba yetu ni jahim, nawe, shetani mcheshi,
Kiipokonya kidogo ladha yake ya udufu.
Walakini buriani: pokea dukati hii:
Na tena, Launseloti, pindi za kula jioni
Utamwona Lorenzo, mgeni wa bwanao mpya:
Kampe barua hii; na mpe kisirisiri;
Basi sasa buriani: sitaki baba aone
Nikizungumza nawe.

LAUNSELOTI: Buriani! machozi yanaurudi ulimi wangu. Mpagani mzuri kupita wote, Yahudi mwema kupita wote! Kama Mkristo hatajifanya mpumbavu ili akupate basi nimedanyanyika. Lakini, buriani: matone haya ya

upambavu yanazamisha kidogo moyo wangu wa kiume: buriani.

JESSIKA: Kwa heri ya kuonana, Launseloti mwema.

(*Launseloti anatoka*)

Ole wangu, nina dhambi gani mbaya ndani yangu,
Kufanya nione haya kuwa mwana wa babangu!
Ila ningawa bintiye wa damu, si wa tabia.
O, Lorenzo, ukiweza kutimiza ahadiyo,
Nitatia kaditama kwenye mashindano haya,
Niwe mkeo mpenzi kisha kuwa Masihiya!

(*Anatoka*)

II . 4

Bado Venisi. Barabarani

(*Aingia Gratiano, Lorenzo, Salarino na Salanio*)

LORENZO: La, tutanyata wakati wa chakula cha jioni
Tukajigeuze kwangu turudi kwa saa moja.

GRATIANO: Na bado hatujafanya matayarisho mazuri.

SALARINO: Hatujasema juu ya wabebaji wa mienge.

SALANIO: Ni mbaya sana, ila iratibiwe vizuri,
Bali ni bora, nadhani, kuiachilia mbali.

LORENZO: Sasa saa kumi: tuna saa mbili kuandaa.

(*Aingia Launseloti ana barua*)

Rafiki Launseloti, je kuna habari gani?

LAUNSELOTI: Yaelekea kuwa itakupendeza kupasua hii.

LORENZO: Naufahamu mkono: na ni mkono mzuri;
Mkono ulioandika ni mweupe kuuzidi
Weupe wa karatasi uloandika juuye.

GRATIANO: Habari ni za mahaba.

LAUNSELOTI: Uniwie radhi, bwana.

LORENZO: Unaelekea wapi?

LAUNSELOTI: Hakika, bwana, nakwenda kumkaribisha bwana wangu wa zamani Yahudi, akale kwa bwana

wangu mpya Mkristo.
LORENZO: Chukua, chukua hizi: (*anampa fedha*)
Mwambie Jessika mwema
Asiwe na shaka kamwe; mwambie kisirisiri.
(*Launseloti anaondoka*)
Nenda: Enyi waungwana, je mmejitayarisha
Kwa vichekesho jioni? Mimi n'na mshika mwenge.
SALARINO: Naam, hakika nakwenda mara kujiandaa.
SALANIO: Na mimi pia nakwenda.
LORENZO: Njoo kwa Gratiano, nitakuwa naye kwake
Baada ya saa moja hivi kuanzia sasa.
SALARINO: Ni vizuri tukifanya hivyo.
(*Salarino na Salanio wanaondoka*)
GRATIANO: Barua hiyo si ya kutoka kwa Jessika mwema?
LORENZO: Sina budi nikwambie mipango yote ilivyo.
Keleza n'tavyomtoa nyumbani kwa baba yake;
Vile vile na dhahabu na vitu alivyo navyo;
Na vazi la mtumishi alilolitayarisha.
Kama Yahudi babaye ataingia mbinguni,
Itakuwa ni sababu ya binti yake mpole:
Na baa halithubutu kumgusa mwali huyu,
Ila kwa kusingizia kwamba linafanya hivyo
Kwa kuwa yeye ni binti wa kafiri Myahudi.
Njoo, fuatana nami: soma hii tukienda;
Mimi cheupe Jessika ndiye atakayekuwa
Mshikaji mwenge wangu.
(*Wanatoka*)

II . 5

Venisi Bado. Mbele ya nyumba ya Shailoki

(*Aingia Shailoki na Launseloti*)

SHAILOKI: Haya vema, utaona, mwenyewe utaamua,
Baina ya Shailoki mzee na Bassanio:—

Hebu, Jessika!—Na huko 'sifanye ulafi wako
Ulivyolafua kwangu;—Wapi, Jessika!—Jessika!—
Na kulala, kukoroma na kurarua mavazi;—
Wapi, Jessika; naita!

LAUNSELOTI: Wapi, Jessika, naita!

SHAILOKI: Kakwambiani kuita? Sikukwambia kuita.

LAUNSELOTI: Mheshimiwa, ulipenda kunambia kuwa sifanyi lolote bila kuambiwa.

(*Aingia Jessika*)

JESSIKA: Umeita? Ni nini mapenzi yako?

SHAILOKI: Nimekaribishwa nende nikale nje, Jessika:
Funguo zangu ni hizi: bali nakwenda kwa nini?
Sikuitwa kwa mapenzi; wanajipendekeza tu:
Walakini hata hivyo, nitakwenda kwa karaha,
Nikamle Masihiya mbadhirifu wa mali.
Jessika, kijana wangu, angalia nyumba yangu.
Nakwenda na sebusebu na kijoyo nacho kimo.
Kuna maovu fulani yanayoninyemelea,
Kwani leo niliota mafurushi ya mapesa.

LAUNSELOTI: Nakusihi, bwana, nenda; bwana wangu mpya anangojea kufika kwako.

SHAILOKI: Nami nangojea yake.

LAUNSELOTI: Na wamefanya njama,—sisemi kwamba utaona vinyago; lakini ukiviona, basi itakuwa si bure pua yangu ilipoanza kutoka damu siku ya Jumatatu—Nyeusi iliyopita, saa kumi na mbili asubuhi iliyotokea mwaka huo Jumatano ya Majivu ilikuwa miaka minne adhuhuri.

SHAILOKI: Wambaje, kuna vinyago? Nisikilize, Jessika:
Ifunge milango yangu; na usikiapo ngoma
Na sauti mbaya sana za mpigaji filimbi
Mwenye shingo ilopinda usipande madirisha,
Wala usitoe kichwa chako mabarabarani,
Kuwaona Masihiya wapumbavu wapitao
Wenye nyuso rangi-rangi. Bali funga masikio,

Ya'ni funga madirisha yote ya nyumbani kwangu:
Usiachie sauti ya ulimbwende hafifu
Iingie nyumba yangu tulivu. Kweli, naapa,
Kwa kongojo la Yakobo moyo wangu haupendi
Nikale nje kwa leo: walakini nitakwenda.
Kanitangulie, wee! Waambie nitakuja.

LAUNSELOTI: Nitatangulia, bwana. Bibi mdogo, pamoja na yote haya tazamia hili nje:

Atapita Masihiya,
Ambaye nakuahidi,
Jicho la binti Yahudi
Litamwona ni hedaya.

(*Anatoka*)

SHAILOKI: Asemaje mjinga huyo mwana wa Hagari, Ha?

JESSIKA: Manenoye yalikuwa, ni kwa heri, bibi, basi.

SHAILOKI: Baradhuli ana wema, ila anakula mno,
Kwenye kazi ya faida bozi kama konokono;
Anasinzia mchana kumzidi paka shume:
Sipatani na wavivu; kwa hiyo nimemwachia:
Na tena nimemwachia kwa ambaye ningependa
Amwauni kuharibu utajiri wa kukopa.
Vema, Jessika, ingia: huenda nirudi mara:
Fanya nilivyokwambia: ujifungie kwa ndani;

Mfunga imara hapati hasara,
Ni methali bora na yenye busara.

(*Anatoka*)

JESSIKA: Kwa heri: na bahati yangu isiponichezea,
Mimi nina baba, wewe binti, aliyepotea.

(*Anatoka*)

II . 6

Bado Venisi. Mbele ya nyumba ya Shailoki

(*Aingia Gratiano na Salarino wamevaa vinyago*)

GRATIANO: Hapa ndipo upenuni pale ambapo Lorenzo
Alitaka tusimame.
SALARINO: Saa yake inakwisha.
GRATIANO: Ni ajabu kachelewa, wapenzi huwahi mno.
SALARINO: O, tetere wa Zuhura hwenda kasi mara kumi,
Kuthibitisha mapenzi yalofanywa punde hivi,
Kuliko kuwa mwamana kwa ahadi ya zamani.
GRATIANO: Ndivyo ilivyo daima: nani huacha karamu
Ana hamu ile ile kama aloanza nayo?
Na yuko wapi farasi azirudiaye tena
Hatuaze za uchovu kwa harara ile ile,
Alokimbilia kwanza? Vitu vyo vyote vilivyo,
Vina moyo kukimbizwa kuliko kujipendeza.
Itokapo bandarini, merikebu ilopambwa,
Huwa mithili kijana au kama mfujaji,
Huwa imekumbatiwa na upepo mtukutu!
Na wakati wa kurudi hurudi imefujika;
Mataruma machakavu na matanga matatuke;
Imetota, mufilisi, kwa upepo mtukutu!
SALARINO: Lorenzo ni huyu aja: haya zaidi halafu.

(*Aingia Lorenzo*)

LORENZO: Marafiki wema, kunradhini kwa kuchelewa.
Si mimi, ni kazi zangu, zilizowangojesheni:
Na nyie mtapocheza kupata wake kwa wizi
Mimi pia sitaacha kutazama. Karibuni:
Hapa ndipo maskani ya baba yangu Yahudi.
Hodi? Kuna nani ndani?

(*Aingia Jessika, juu, kavaa nguo za kiume*)

JESSIKA: Nani wewe? Niambie nihakikishe zaidi,

Japo naweza kuapa nakujua kwa sauti.
LORENZO: Lorenzo, kipenzi chako.
JESSIKA: Ndiyo Lorenzo hakika, na kipenzi changu kweli;
Ninayempenda hivi? Na ni nani ajuaye
Isipokuwa Lorenzo kama nimekuwa wako?
LORENZO: Mbingu na mawazo yako ni mashahidi u wangu.
JESSIKA: Haya, shika kasha hili; lafidia ta'bu hizi.
Nafurahi ni usiku na huwezi kuniona,
Maana naona haya hivi nionekanavyo:
Bali penzi ni kipofu, na wapenzi hawaoni
Makosa madogodogo wayafanyayo wenyewe;
Maana wangeyaona hata mungu wa mapenzi
Angefadhaika sana kuniona mvulana.
LORENZO: Telemka, kwa sababu utanishikia mwenge.
JESSIKA: Nini, nishike kimuli, nimulike haya zangu?
Ambazo pasipo taa zinaonekana sana.
Kumbe, shughuli zenyewe ni uvumbuzi, kipenzi,
Na mimi wajibu wangu yanipasa kujificha.
LORENZO: Umefichika kipenzi, kwa vazi la kivulana.
Bali telemka hima; usiku unakimbia
Nasi tumesha chelewa karamu ya Bassanio.
JESSIKA: Kwanza nifunge mlango, na nijiongeze fedha,
Kisha nitakuja mara.

(*Anatoka*)

GRATIANO: Kweli, kwa kinyago changu, ni Pagani,
Si Yahudi.
LORENZO: Ole wangu, nampenda kwa mtima wangu wote;
Sababu ana hekima, kadiri nimuonavyo:
Tena ni mzuri sana, kama naona vizuri;
Vile vile ni mkweli, kama alivyoonyesha;
Na kwa hiyo, vivyo hivyo yeye mwenyewe alivyo
Mwenye hekima, mzuri, na tena mwenye ukweli,
Ndivyo atakavyokuwa daima moyoni mwangu.

(*Aingia Jessika chini*)

Aa, umekuja? Haya, waungwana, twende zetu!
Wenzi wetu wachezaji hivi sasa watungoja.

(*Wanatoka na Jessika na Salarino*)

(*Aingia Antonio*)

ANTONIO: Nani huyo?

GRATIANO: Bwana Antonio?

ANTONIO: Hima, hima, Gratiano! Wengine wote wa wapi?
Ni saa tatu; wageni wote wawangojeeni.
Leo hakuna vinyago: pepo zimebadilika;
Bassanio 'taondoka mara kuenda chomboni.
Nimetuma ishirini watu kuwatafuteni.

GRATIANO: Nafurahi kusikia hivyo: sina nipendacho
Kupita kutweka tanga na kwenda usiku huu.

(*Wanatoka*)

II · 7

Belimonti. Chumbani, kwa Poshia

(*Mlio wa Tarumbeta. Aingia Poshia pamoja na Mwana wa Mfalme wa Moroko na wafuasi wao*)

POSHIA: Kayavute mapazia masanduku yaoneke
Kwake mtukufu huyu mtoto wa mfalme.
Haya sasa kachague.

MOROKO: La kwanza, ni la dhahabu, lenye maandiko haya:
'Anichaguaye mimi atakuwa amepata
Kile wanaume wengi wakitamanicho sana.'
Na la pili, ni la fedha, linaloahidi hivi:
'Anichaguaye mimi apate astahilicho.'
La tatu, risasi butu, na onyo lake ni butu:
'Anichaguaye mimi itambidi atoe,
Na pia ahatirishe cho chote alicho nacho.'
Nitajuaje ya kuwa nimechagua vizuri?

POSHIA: Moja lina picha yangu, mzawa wa mfalme:

Ukilichagua hilo basi na mimi ni wako.
MOROKO: Muungu fulani uniongoze. Hebu nione;
Nitayachungua tena maandiko toka mwisho.
Nitaanzia la tatu: lasemaje, la risasi?
'Anichaguaye mimi itambidi atoe
Na pia ahatirishe cho chote alicho nacho.'
Itambidi atoe—atoleeni? Risasi?
Na pia ahatirishe—kwa ajili ya risasi?
Sanduku hili latisha: wahatirishao vyote
Hutumaini kupata faida iliyo nzuri:
Wenye moyo wa dhahabu hawajali takataka;
Kwa hiyo basi sitoi na wala sihatirishi
Cho chote nilicho nacho kwa sababu ya risasi.
La fedha lasema nini, lenye rangi ya baridi?
'Anichaguaye mimi apate astahilicho.'
Apate astahilicho! Subiri hapa, Moroko.
Upime thamani yako kwa mkono mwadilifu:
Kama ukithaminiwa vile ujifanidivyo
Wastahili kutosha; walakini ya kutosha
Inaweza isitoshe kumpata siti huyu.
Bali nikitia shaka kuwa simstahili,
Basi hapo nitakuwa najiumbua mwenyewe.
Stahili yangu ni nini? Bila shaka ni bibie.
Namstahili, hakika, kwa nasaba na kwa mali,
Kwa madaha na kwa sifa zote za malezi mema;
Na kuzidi yote hayo namstahili kwa pendo.
Vipi, nisiendelee, nichague papa hapa?
Hebu tuyaone tena ya sanduku la dhahabu:
'Anichaguaye mimi atakuwa amepata
Kile wanaume wengi wakitamanicho sana!'
Naam, ni siti huyu; anotamaniwa kote.
Toka pande zote nne za dunia wanakuja
Kubusu sanamu hii takatifu ilo hai:
Majangwa ya Hirikani na nyika pana ajabu,

Za Uarabuni kote, sasa zimekuwa njia
Ziletazo watawala kumwona Poshia bora.
Nayo dola ya bahari ambayo inapofura
Hutemea hata mbingu, haiwezi kuzuia
Nia ya wageni hao; ila wanazidi kuja,
Kama wavuka kijito, kumwona Poshia bora.
Moja la matatu haya lina picha yake nzuri.
Itawezekana kweli liwe lile la risasi?
Wazo chafu kama hilo lingekuwa ni laana.
Halifai japo kuwa sanda yake kaburini.
Au niwaze ya kuwa kawekwa ndani ya fedha?
Moja ya kumi na moja ya thamani ya dhahabu?
Hilo ni wazo la dhambi! Kito cha thamani hivi
Hakiwekeki po pote ila ndani ya dhahabu.
Uingereza wanayo sarafu tu ya dhahabu,
Ambayo kwa juu yake imechapwa malaika.
Bali hapa malaika mwenyewe hasa yu ndani
Ya sanduku hili hapa. Niletee ufunguo:
Basi n'tachagua hapa, na bahati nijaliwe!

POSHIA: Ni huu hapa, chukua, mzawa wa mfalme;
Kama sura yangu imo nimekuwa mali yako.

(*Anafungua sanduku la dhahabu*)

MOROKO: Mama yangu! Nini hii? Ni fuu tupu la kichwa,
Ambalo katika jicho lina hati ya ma'ndiko.
Nitasoma maandiko.
'Kila kitu king'aacho usidhani ni dhahabu,
Umekisikia hicho ni kiambo cha mababu.
Kuniona kwa nje tu, wengi wameuza utu;
Makaburi ya dhahabu yana mafunza ajabu.
Ungekuwa na werevu ulivyo na ushupavu,
Kijana kiwiliwili na mzee kwa akili,
Usingelistahili kulipewa jibu hili:
Basi buriani dawa; posa umefarikiwa.'
Nimefarikiwa kweli. Bure nimejitanibu.

Basi buriani, joto; nawe, makiwa, karibu.
Basi, kwa heri Poshia. Ninayo huzuni sana
Siwezi kwa heri ndefu: Ndivyo wanavyoagana
Watu waliopoteza.

(*Anaondoka na Wafuasi wake. Tarumbeta*)

POSHIA: Ni kuvuja kwa pakacha. Yuta pazia. Nendeni.
Wote wamfananao, wachague vivyo hivyo.

(*Anatoka*)

II · 8

Venisi. Barabarani

(*Aingia Salarino na Salanio*)

SALARINO: Ndiyo, yahe, nimemwona Bassanio kesha tweka:
Pamoja naye anafuatana na Gratiano.
Na sina shaka Lorenzo hayumo chomboni mwao.

SALANIO: Kisirani Myahudi 'limwamsha Sultani'
Kwa ghasia na kelele, waende wakatafute
Melini kwa Bassanio.

SALARINO: Alichelewa lakini, meli ilisha kutweka:
Bali kule Sultani alifahamishwa kuwa
Lorenzo na kipenziye Jessika walioneka
Wamo ndani ya gondola. Aidha, na Antonio,
Alithibitisha kuwa hawakuwamo chomboni
Pamoja na Bassanio.

SALANIO: Sijapata kusikia makelele ya ajabu,
Ya kiovu, mara hivi, mara vile, kama hayo.
Huyu mbwa Myahudi kalia barabarani:
Binti yangu!—O, dukati zangu! O, binti yangu O!
Kakimbia na Mkiristo! Dukati zangu Kristo.
Oo, haki! O, Sheria! Dukati zangu na binti!
Mfuko uliofungwa, miwili iliyofungwa!

Ya dukati maradufu, kanibia binti yangu!
Pamwe na vito, viwili, viwili vya tunu kubwa,
Kaviiba binti yangu! Haki! Leta mwali huyu!
Anazo johari hizo, pamwe na dukati pia.

SALARINO: Basi, wavulana wote wa Venisi wamwandama
Alilia vito vyake, binti yake na dukati.

SALANIO: Basi, Antonio mwema aitimize shahada
Ama sivyo, ataona kisa cha mtema kuni.

SALARINO: Hasa umetanabahi: Jana nilizungumza
Na Mfaransa mmoja, alonambia ya kwamba
Kwenye mlangobahari utengao Wafaransa
Na watu wa Uingereza imeangamia meli
Iliyojaa shehena, nayo ni ya nchi yetu;
Aliponambia hayo nilimwaza Antonio,
'Kiomba kimoyomoyo isije kuwa ni yake.

SALANIO: Ingefaa umwambie hayo uliyosikia:
Bali 'sifanye haraka, aweza kuhuzunika.

SALARINO: Mtu mwema kumzidi hako katika dunia;
Niliona Bassanio na yeye wakiagana:
Bassanio alisema atarudi kwa haraka:
Na yeye akamjibu: 'Hasha, usifanye hivyo;
Usiharibu shughuli juu yangu, Bassanio,
Bali kaa hadi mwisho; na habari ya shahada
Aliyo nayo Yahudi juu yangu usiwaze;
Usiache iingie akilizo za mahaba:
Cheka na kuchangamka: na fikara zako kubwa
Ziwe juu ya uchumba na kuonyesha mapenzi
Itakavyohitajika na kukulaiki kule.'
Basi hapo, macho yake yamevimba kwa machozi,
Akageuza usowe, akatoa mkonowe
Kwa nyuma, na kwa mapenzi makubwa sana ajabu
Kushika wa Bassanio; na hivyo wakaagana.

SALANIO: Nadhani kuwa dunia aipendeaye tu.
Tafadhali twende zetu tumtafute aliko.

Ili tumpunguzie uzito wa moyo wake,
Kwa kitulizo cho chote.
SALARINO: Twende tukafanye hivyo.
(*Wanatoka*)

II . 9

Belimonti. Chumba katika nyumba ya Poshia

(*Aingia Nerissa na Mtumishi*)

NERISSA: Fanya hima, tafadhali; vuta pazia upesi:
Mwana wa Mfalme wa Arragoni kesha apa,
Naye aja sasa hivi kuja kujichagulia.
(*Tarumbeta zalia. Aingia Mwana wa Mfalme Arragoni, Poshia na wafuasi wao*)
POSHIA: Angalia, mtukufu Mzawa wa Mfalme,
Wayaona yale pale ni masanduku matatu,
Kama ukilichagua lile ambalo nilimo,
Papo zitaadhimishwa ibada za ndoa yetu:
Walakini ukishindwa, papo hapo, bwana wangu,
Bila maneno zaidi, utapaswa kuondoka.
ARRAGONI: Ninapaswa kwa kiapo kufanya mambo matatu:
La kwanza, nisimwambie mtu mwingine ye yote,
Sanduku nilochagua; na la pili, nikishindwa,
Daima nisimpose mwali ye yote kwa ndoa;
Na la tatu, nikishindwa, niondoke pale pale.
POSHIA: Masharti yote haya yampasa kila mtu
Anokuja kujaribu kunipata duni mimi.
ARRAGONI: Nami pia ni tayari kuyatimiliza hayo.
Sasa, Bahati, ridhisha matumainio yangu!
Dhahabu, fedha, risasi nayo ya thamani duni.
Anichaguaye mimi itambidi atoe
Na pia ahatirishe cho chote alicho nacho.'
Utapaswa upendeze kuzidi hivyo ulivyo,
Ndipo nitoe cho chote au nikihatirishe.

Na sanduku la dhahabu lasemaje? Ha! nione:
'Anichaguaye mimi atakuwa amepata
Kile wanaume wengi wakitamanicho sana.'
Kile wanaume wengi wakitamanicho sana!
Ile 'wengi' inaweza ikawa ni kina yahe
Wale wanaochagua kwa kuona nje tu,
Wasojifunza zaidi kuzidi wayaonayo;
Wasioona kwa ndani, mithili ya ndege yule
Anayejiweka nje na kujenga ukutani
Hata kama ni njiani na shabaha ya ajali:
Mimi kamwe sichagui wengi wanachotamani,
Kwani sitarukaruka pamoja na kina yahe,
Na kujifanya ni sawa na makundi ya kishenzi.
Kumbe, basi, ni wewe tu, ewe dafina ya fedha;
Nambie mara nyingine maandiko ulonayo:
'Anichaguaye mimi apate astahilicho.'
Na imesemwa vizuri; kwani nani atakwenda
Kuidanganya bahati na abaki na heshima
Ikiwa hastahili? Asithubutu ye yote
Kujivisha utukufu asioustahili.
Laiti kama heshima, na utukufu na vyeo
Visingalipatikana kwa njia ziso za haki!
Kama heshima ng'aavu ingenda kwa mwenye haki
Wangeipata wangapi ambao hawana kitu?
Wangapi waamuruo wangeamriwa wao!
Ni wakulima wangapi walo na hali za chini
Wangeweza kuoneka kwenye viti vya heshima!
Na heshima gani hiyo ingeweza kuokotwa
Kwenye kapi na katika takataka za nyakati,
Ipigwe msasa upya! Vema, nijichagulie:
'Anichaguaye mimi apate astahilicho.'
Nachukua haki yangu. Nipe ufunguo wake,
Na mara nifungulie, bahati yangu ya hapa.

(*anafungua sanduku la fedha*)

POSHIA: Kusita kurefu mno kwa hicho ulichopata.
ARRAGONI: Nini hii? Ni sanamu ya mjinga hayawani,
Inanipa maàndiko! Ambayo nitayasoma.
Tofauti gani hiyo kati yake na Poshia!
Tofauti gani kati yake na matumaini
Niliyokuwa ninayo na kustahili kwangu!
'Anichaguaye mimi apate astahilicho.'
Sikustahili zaidi ya kichwa cha hayawani?
Hilo ndilo tuzo langu? Sina stahiki bora?
POSHIA: Kuudhi na kuhukumu ni shughuli mbalimbali,
Na tena ni tofauti.
ARRAGONI: Ni nini kilicho hapa?
(*Anasoma*) 'Kwenye moto mara saba hii imejaribiwa,
Hiyo hiyo mara saba imethibitika kuwa
Hekima ya kweli kweli ni kuchagua vizuri—
Kuchagua kwa akili: hiyo ndiyo tabasuri.
Kuna watu wapendao vivuli kukumbatia;
Thawabu ya watu hao nayo ni vivuli pia.
Nafahamu kwa hakika kuna watu wapumbavu,
Kwa nje wamejipaka fedha, tena wang'aavu.
Ni kadhalika na hili, la kichwa cha baradhuli.
Sasa daima dawamu nitakuwa kichwa chako,
Huna nyingine nujumu: umekwisha; nenda zako.'
Nitaonekana kuwa ni mpumbavu zaidi,
Nikizidi kuchelewa na kufanya ukaidi.
Kuposa nilipokuja nilikuja nina kichwa
Cha mpumbavu mmoja: pamwe na kilichofichwa
Ninarudi na viwili; na vyote vya baradhuli.
Basi, bibi, buriani. Nitatimiza ahadi,
Nivumilie moyoni ghadhabu bila inadi.
(*Arragoni na Wafuasi wake wanaondoka*)
POSHIA: Hivyo ndivyo mshumaa ulivyomwunguza nondo.
Wajinga hawa hubwata! Wakianza kuchagua
Akili wanazopata maarifa huwavua.

NERISSA: Methali ya kale ile ni kweli si ya kuzua,
Kifo na mke, yambile, si kuchagua, ni tua.
POSHIA: Haya basi, twende zetu, vuta pazia, Nerissa.
(*Aingia Mtumishi*)
MTUMISHI: Yuko wapi bibi mwana?
POSHIA: Hapa: nini, maulana?
MTUMISHI: Bibi, mlangoni kuna kijana wa Kivenisi
Anayemtangulia bwanaye alo njiani.
Tena kaja na salamu ambazo zinalambika,
Ya'ni pamoja na sifa na maneno ya heshima
Kaja na zawadi bora. Sijapata kumuona
Mchukuzi wa mapenzi kupendeza kama huyu:
Na siku ya Aprili haijapendeza hivyo
Kutambulisha uzuri wa kaskazi ijayo,
Alivyo mjumbe huyu akidamuye bwanaye.
POSHIA: Yametosha, tafadhali: Ukiendelea hivyo
Sasa hivi utasema kuwa ni jamaa yako.
Unabadhiri akili kumsifu mtu huyu.—
Njoo, twendeni, Nerissa; natamani kumuona
Tume wa mapenzi huyo ajaye kwa utu hivyo.
NERISSA: Ewe habab Mapenzi, penda awe Bassanio!
(*Wanatoka*)

III · 1

Venisi. Barabarani

(*Waingia Salanio na Salarino*)

SALANIO: Je, kuna habari gani kutoka Rialitoni.

SALARINO: Eti, na wala haijakanushwa, meli moja ya Antonio, iliyojaa shehena ya thamani kubwa, imeangamia katika mlangobahari; mahali panapoitwa Gudiwini, nadhani; mahali pa hatari na pafishaji sana, ambapo pana mizoga mingi ya meli kubwa kubwa; ikiwa maneno yangu, kama wasemavyo, ni kama maneno ya mwanamke msema kweli.

SALANIO: Natumaini ni maneno ya mwanamke mwongo kama mwanamke aliyewaongopea majirani zake kwamba alilia alipofiwa na mume wake wa tatu. Lakini ni kweli, bila kusema maneno mengi mno au kuzidi mpaka wa mazungumzo, kwamba Antonio mwema, Antonio mwaminifu, — O, laiti ningeweza kupata neno zuri la kutosha kulaiki jina lake:—

SALARINO: Basi! mwisho! mwisho!

SALANIO: Ha! wasema nini? Ala, mwisho ni kuwa kapoteza meli.

SALARINO: Ningependa iwe ndiyo mwisho wa hasara zake.

SALANIO: Acha niseme amina mapema, kabla shetani hajapinga sala yangu; maana namwona anakuja ana sura ya Yahudi.

(*Aingia Shailoki*)

Hali gani, Shailoki? Habari gani za wafanya biashara?

SHAILOKI: Ulifahamu, kuzidi ye yote, kuzidi mtu mwingine ye yote, wewe ulifahamu kuwa binti yangu katoroka.

SALARINO: Hiyo ni kweli kabisa. Mimi, kwa upande wangu nilijua mshonaji aliyemshonea mabawa ya kurukia.

SALANIO: Na Shailoki naye, kwa upande wake, alimjua ndege mwenye manyoya; nayo ni maumbile yao kuliacha bwawa.

SHAILOKI: Na apate baa kwa ajili hiyo.

SALARINO: Hiyo ni wazi akihukumiwa na Shetani.

SHAILOKI: Mwili wangu na damu yangu mwenyewe kuasi!

SALARINO: Kuna tofauti kubwa zaidi kati ya mwili wake na wako kuliko kati ya jiwe jeusi na jino la tembo; tofauti zaidi kati ya damu zenu kuliko tofauti iliyopo kati ya mvinyo mwekundu na mvinyo wa Rhine. Lakini hebu twambie, una habari kama Antonio kapata hasara baharini au sivyo?

SHAILOKI: Sasa nina mapatano mengine mabaya; mfilisika mbadhirifu, ambaye hathubutu kutokeza kichwa chake katika Rialito; kibapara ambaye alikuwa akija sokoni kwa maringo; aangalie shahada yake: alipenda kuniita mla riba; n'aangalie shahada yake: alipenda kuazima mapesa kwa jamala ya Kikristo; n'aangalie shahada yake.

SALARINO: Nini, nina hakika kuwa asipoitimiza huwezi kumkata nyama: itakufaa nini?

SHAILOKI: Kuvulia samaki: kama haiwezi kulisha kitu cho chote, itaweza kulisha kisasi changu. Amenifedhehesha, amenizuia kupata nusu milioni; amenicheka kwa kupata hasara, amenikejeli kwa kupata faida, amenyanyasa kabila langu, amepinga mikataba yangu, amepooza marafiki zangu, amechochea maadui zangu; na sababu yake ni nini? Kwa kuwa mimi ni Yahudi. Yahudi hana macho? Yahudi hana mikono, hana viungo, hana vimo, hana akili, hana upendo au shauku? Hali chakula kile kile, hajeruhiwi na silaha zile zile, haugui magonjwa yale

yale, hatibiwi kwa njia zile zile, hapati joto au baridi kwa majira yale yale kama Mkristo? Mkituchoma, hatutoki damu? Mkitutekenya, hatucheki? Mkitulisha sumu, hatufi? Na mkitukosea, tusilipize kisasi? Kama sisi na nyinyi tunafanana katika yale mengine, basi tunafanana katika hilo pia. Kama Yahudi akimkosea Mkristo saburi yake ni nini? Kisasi: Kama Mkristo akimkosea Yahudi ustahimilivu wake uwe nini kwa kufuata mfano wa Kikristo? Bila shaka, kisasi. Maovu mnifundishayo nitayatekeleza; na itakuwa ngumu lakini nitatoa mafunzo mazuri zaidi.

(*Mtumishi anaingia*)

MTUMISHI: Waungwana, bwana wangu Antonio yuko nyumbani kwake na angependa kuzungumza na nyinyi wote wawili.

SALARINO: Tumekwenda huko na huko tukimtafuta.

SALANIO: Naona mkabila mwingine anakuja: wa tatu hatakuwa na kifani, ila labda shetani mwenyewe awe ni Yahudi.

(*Wanatoka Salanio, Salarino na Mtumishi*)

(*Aingia Tubali*)

SHAILOKI: Je, Tubali! Habari gani kutoka Genoa? Umempata binti yangu?

TUBALI: Mara nyingi nilifika mahali niliposikia habari juu yake, lakini sikumpata.

SHAILOKI: Ah, ah, ah, ah, alimasi imekwenda, ilinigharimu dukati elfu mbili huko Frankifuti! Laana haikufikia taifa letu mpaka sasa; sikupata kuijua laana hiyo mpaka sasa: dukati elfu mbili ndani yake; na vito vingine vyenye thamani. Afadhali binti yangu angekuwa ni mauti chini ya miguu yangu na vito anavyo masikioni mwake! Afadhali angekuwa kalala miguuni pangu na dukati ziko ndani ya jeneza! Hakuna habari yo yote juu ya johari zangu? Haya, basi: na wala sijui gharama ya kuzitafuta: lo,

wewe hasara juu ya hasara! mwizi kenda na kiasi fulani, halafu kiasi fulani cha kumtafuta mwizi; bila kupata cho chote, bila kulipa kisasi: wala hakuna mkosi usiokuwa wangu; hakuna kitu cha majonzi ila ni changu; na machozi yote ni yangu.

TUBALI: Naam, watu wengine pia wana bahati mbaya: Antonio, kama nilivyosikia huko Genoa,—

SHAILOKI: Nini, nini, nini? Bahati mbaya, bahati mbaya!

TUBALI: Meli yake moja imeteketea, ikija kutoka Tripoli.

SHAILOKI: Namshukuru Mungu, namshukuru Mungu! Ni kweli, ni kweli?

TUBALI: Nilizungumza na baadhi ya mabaharia waliosalimika kutoka katika meli hiyo.

SHAILOKI: Nakushukuru, Tubali mwema: habari njema, habari njema! ha, ha! wapi? Genoa?

TUBALI: Nasikia kwa usiku mmoja tu binti yako alitumia dukati themanini mjini Genoa.

SHAILOKI: Unanichoma kwa jambia; sitaona dhahabu yangu kamwe: dukati themanini katika kikao kimoja! dukati themanini!

TUBALI: Nilikutana na wadai wengi wa Antonio kule Genoa ambao walisema kuwa lazima ashindwe kutimiza shahada yake.

SHAILOKI: Nafurahi sana kusikia hivyo; nitamwandama; nitamtesa; nafurahi sana kusikia hivyo.

TUBALI: Mmoja wao alinionyesha pete aliyopewa na binti yako kwa tumbili.

SHAILOKI: Alaaniwe! Unanitesa, Tubali, ni kile kito changu cha Kituruki. Nilikipewa na Leah nilipokuwa sijaoa: nisingeweza kukitoa kwa msitu mzima wa tumbili.

TUBALI: Lakini Antonio amekwisha hakika.

SHAILOKI: Naam, hiyo ni kweli, ni kweli kabisa, nenda, Tubali, nilipie afisa mmoja, sema naye majuma mawili

kabla. Akishindwa, nitatwaa moyo wake. Kwani, kama akiondoka Venisi naweza kufanya biashara yo yote nipendayo. Nenda, Tubali, tukutane kwenye Sinagogi letu. Nenda Tubali, mwema, kwenye Sinagogi letu, Tubali.

(*Wanatoka*)

III . 2

Belimonti. Chumba katika nyumba ya Poshia

(*Aingia Bassanio, Poshia, Gratiano, Nerissa na Watumishi*)

POSHIA: Nakusihi, usubiri: siku moja au mbili,
Kabla ya kuchagua; maana ukikosea,
Na mimi nitakukosa; basi, subiri kidogo.
Kuna kitu chanambia--lakini siyo mapenzi
Ya kuwa nisikukose; na wewe unatambua
Kwamba chuki haitoi mashauri kama hayo.
Lakini ili usije kunielewa vibaya—
Bali mwanamwali hana ulimi, ila mawazo—
Ningelikuweka hapa mwezi, pengine miwili,
Ndipo unibahatishe. Hata ningekufundisha
Uchague jinsi gani; lakini nimeapishwa;
Basi sitakufundisha: na waweza kunikosa.
Lakini ukinikosa naweza tamani dhambi,
Kuwa nisingaliapa. Ole wangu, macho yako
Ni zama yameniroga, na yamesha kunigawa;
Nusu yangu moja yako, ya pili pia ni yako,—
Yangu mwenyewe, niseme; na kama yangu, ni yako,
Kwa hiyo zote ni zako! O, nyakati mbaya hizi,
Zitiazo pingamizi kati ya wenye na vyao!
Na kwa hiyo japo wako, si wako: ithibitishe,
Iangamie bahati, nisiangamie mimi.
Nasema kirefu mno; ni kupitisha wakati,

Kuukuza na kufanya uwe mrefu zaidi,
Uchelewe kuchagua.

BASSANIO: Niachie nichague.
Kwani sasa nafanana na ateswaye mekoni.

POSHIA: Na ateswaye mekoni, Bassanio! iungame
Salata ilochanganywa pamoja na mapenziyo.

BASSANIO: Hapana salata kamwe ila ile ya mashaka
Inofanya nahofia kufaidi penzi langu:
Ingelikuwa rahisi 'kina theluji na moto
Kupendana kirafiki au kuishi pamoja
Kuliko salata kuwa pamoja na penzi langu.

POSHIA: Ndiyo, lakini wasema kama aliye mekoni,
Watu walazimishwako kusema kitu cho chote.

BASSANIO: Niahidie maisha, nitaungama ukweli.

POSHIA: Basi, ungama uishi.

BASSANIO: Ungama na ukapenda
Ndiyo ingekuwa hasa kuungama kwangu kote:
O, mateso ya furaha, yule anayenitesa
Anaponielekeza majibu ya ukombozi!
Bali acha nifuate bahati na masanduku.

(*Pazia linavutwa kuonyesha masanduku*)

POSHIA: Haya, basi! Nimo ndani ya mojawapo la hayo:
Ikiwa unanipenda, utagundua nilimo.—
Nerissa, na wengineo, wote simameni kando.—
Utumbuizwe muziki afanyapo uchaguzi;
Basi, kama hakupata, atakwisha kama bata,
Azame kwenye muziki: ili methali ifane,
Macho yangu yatakuwa kijito chake cha mwisho.
Bali hwenda akapata; muziki wa nini, basi?
Na uwe vigelegele wanavyopiga raia
Wanapomsujudia mfalme wao mpya,
Akisha kuvishwa taji: na hivyo ndivyo ulivyo,
Ule muziki mtamu unaopigwa jioni,
Kumwendea sikioni mwotaji bwana arusi,

Kumleta arusini: ndivyo aendavyo sasa,
Hapungukiwi heshima, bali kazidi mapenzi.
Kuzidi Alkide kijana alipomwokoa
Yule mwanamwali hongo liliyopewa dubwana
Na Troi ya majonzi. Mimi ni kama kafara,
Wengine mlio kando ni wakeze Dardano,
Wa sura za kufifia, walokuja kutazama
Matokeo ya pigano. Basi, nenda, Herikule!
Ukiishi, nitaishi: nangoja kwa tashwishi
Matokeo ya pigano kuzidi mwenye pigano.
(*Muziki—huku Bassanio anajisemea mwenyewe juu ya masanduku*)

WIMBO:
Nambie, pendo bandia
Wapi linapoanzia,
Moyoni au kichwani?
Huzaliwa jinsi gani?
Hulelewa jinsi gani?
Nijibu, hima nijibu.
Nalisubiri jawabu.
Macho ndiyo hulizala,
Na chakula ni kulola;
Na hufia pendo hilo
Pa pale penye malalo.
Sote tupige kengele;
Kwa kifo cha pendo lile.
Ninaanza, ngoo, ngoo!

WOTE: Ngoo, ngoo, ngoo, ngoo!

BASSANIO: Basi maono ya nje hayawi vitu vyenyewe:
Dunia dumu daima hudanganywa na mapambo.
Sheriani, ombi gani lingazidi kwa ubaya,
Likipata mtetezi mwenye sauti nyororo,
Halitaficha ubaya? Hata na katika dini,
Kuna dhambi gani mbaya isipate muadhamu

Atakayeibariki na kuikosha kwa aya,
Hivyo afiche maovu kwa mapambo malidadi?
Hakuna ovu lo lote zebezebe kwa kiasi,
Liwe halina cho chote kizuri kwa nje yake.
Kuna waoga wangapi wenye mioyo ya wongo
Kama ngazi za mchanga wanovaa videvuni
Madevu ya Herikule na mungu wa mashujaa,
Wenye maini kwa ndani meupe kama maziwa;
Na hawa hujivalisha kivazi cha mashujaa
Kiwafanyie kigome! Utazame tu uzuri,
Utaona hugharimu uzito wa sawa yake;
Hivyo huwa muujiza kwa yale ya maumbile,
Kuwafanya ni wepesi walio nao kwa wingi:
Na hivyo ndivyo zilivyo na hizo nywele za singa,
Za wazuri wa bandia, na ambazo aghalabu,
Huwa wala siyo zao, bali za vichwa vingine
Vilivyozikuza hizo, sasa vimo kaburini.
Kwa hiyo basi mapambo ndiyo pwani ya ghururi,
Ya bahari ya hatari; ndio ushungi mzuri
Unovaliwa kwa juu ya uzuri wa Kihindi.
Yaani kiinimacho, zikivaacho nyakati,
Kunasa wenye hekima. Basi wewe chaurembo,
Wewe chakula cha Mida, dhahabu, sikuchagui.
Wala wewe kidhabina kati ya mtu na mtu,
Ulofifia kwa rangi: wewe tu, risasi duni,
Wewe unayetishia, bila kuahidi kitu,
Rangi yako yanivuta zaidi ya ufasaha;
Basi, hapa nachagua: shangwe kuwa matokeo!

POSHIA: (*kando*) Jinsi zinavyoyeyuka harara zote hewani,
Kama mawazo ya shaka, na ya kutotumaini,
Ya hofu ya mtetemo na kijicho cha upendo!
O, pendo, fanya kipimo; nikadirie uhondo:
Punguza kiasi chako; ninyeshee kwa uzani!
Yapunguze mafuriko ya mbaraka moyoni,

Nisije nikazimia!
BASSANIO: Nini nionacho hapa?
Ni sura yake kizuri Poshia! Kimungu gani
Amekaribia hivi kuumbika kwa yakini?
Macho haya yajimudu? Au kwa kupanda yangu
Ni kama yanajimudu? Na hii midomo yako
Ambayo imeachana kwa pumzi ya sukari:
Ni kigingi kama hiki chenye haki ya kutenga
Marafiki wa mapenzi. Hapa kwenye nywele zake
Mchoraji kaucheza mchezo wa buibui.
Kaosuku wa dhahabu utando wa kuinasa
Mioyo ya wanaume haraka kuzidi nzi
Anaswavyo utandoni. Walakini macho yake,—
Alipataje uwezo wa kuweza kuyachora?
Kisha kulichora moja nadhani lingaliweza
Kuiba yake mawili libaki halina mwenzi.
Bali ona jinsi gani kusifia kwangu kote
Hakufikii sifaye kama kivuli chenyewe
Kichechemavyo kwa nyuma ya yule mwenye kivuli.
Haya hapa maandiko ambayo yamechukua,
Pia ni muhutasari wa bahati yangu mimi.
(*Anasoma*)
'Wewe usiyechagua macho yanavyokutuma,
Uzidi kuwa na tua, chagua hivi daima!
Kwa kuwa bahati hiyo umebahatiwa wewe
Basi uridhike nayo 'sitafute mwinginewe.
Ikiwa umependezwa nayo unoshikilia
Kama bahati na jezwa, basi sasa geukia
Mwandani wako aliko, na kwa busu la mapenzi
Umchukue, ni wako, wewe ndiye mwenye enzi.'
Maandiko ya raufu.—Bibi mwema kunradhi;
(*Anambusu*)
Nakuja kwa taarifu, kutoa na kukabidhi.
Kama kati ya wawili washindaniao kitu,

Atayepata kibali katika macho ya watu,
Vifijo akisikia, makofi na hekaheka,
Moyo wamzungukia, kashangaa, ana shaka,
Hajui shangwe za watu ni za kwake ama sivyo,
Bibi mwema-mara-tatu, nami ndivyo niimavyo;
Nikingali na mashaka kama haya ni hakika,
Mpaka yamethibitika, sahihi ukiandika.

POSHIA: Waniona niimapo, maulana Bassanio,
Hivi mwenyewe nilivyo: japo kwa ajili yangu
'Singetamani makuu, kupenda nizidi hapa;
Bali kwa ajili yako napenda niwe zaidi,
Ningependa niwe mimi tatu mara ishirini;
Ningeongeza uzuri mara elfu zaidi,
Na mali ningezidisha mara ashara elfu;
Kupata kibali chako ningependa ongezeko
La maadili, uzuri, na mali, na marafiki,
Kuzidi nilivyo navyo; lakini, nilicho nacho
Ni jumla yenye kitu; na ambacho kwa jumla
Ni mwali asiyefunzwa, hakusoma, si mjuzi;
Bali afurahi kuwa kwa sababu si mzee
Ataweza kujifunza; afurahiwa zaidi
Kwamba alivyolelewa hatashindwa kujifunza;
Na kinomfurahisha, kupita vingine vyote,
Ni moyo wake mwanana kujikabidhi kwa wako
Wongozwe kama na bwana, gavana na malikiye.
Mimi na kilicho changu, sasa vyote ni maliyo.
Hadi sasa nilikuwa mwenye jumba zuri hili,
Mwenye watumishi wangu, malikia wa mwenyewe.
Bali sasa, nyumba hii, sasa watumishi hawa
Na huyu mimi mwenyewe, ni mali yako, bwanangu:
Nami navitoa kwako pamoja na pete hii;
Ambayo mkiachana, ukiitoa kwa mtu,
Au ukiipoteza, basi itabashiria
Mwisho wa mapenzi yako, nami nitakulaumu.

BASSANIO: Bibie umeniacha mkavu sina maneno,
Kinachosema na wewe ni damu ya mishipani:
Vipawa vyangu ni vyote vimepigwa bumbuazi,
Kama, ba'da ya hotuba ilotolewa vizuri
Na mwana wa mfalme anayependwa na watu,
Hutokea umatini mungurumo wa furaha;
Ambapo kila kilicho, kwa kuchanganywachanganywa,
Hufanywa kuwa si kitu, ila msitu wa shangwe,
Inosemwa, isosemwa. Walakini pete hii
Iachapo chanda hiki, na uhai uniache:
Basi hapo sema wazi, Bassanio amekufa!
NERISSA: Bwana wangu na bibie, na sasa ni zamu yetu
Tulongoja kujaliwa ombi letu litimizwe,
Kuwatakieni heri: heko, bwana na bibie!
GRATIANO: Bwana wangu Bassanio na bibie muanana,
Nawatakieni heri yote mnayotamani,
Kwani najua yakini hamtanipunguzayo:
Na hapo waheshimiwa mtakapoadhimisha
Muafaka wa imani yenu ninawaombeni
Nami pia hapo hapo nifanye yangu arusi.
BASSANIO: Na kwa moyo wangu wote, kama utapata mke.
GRATIANO: Nakushukuru bwanangu umesha kunipatia.
Macho yangu, bwana wangu, ni mepesi kama yako:
Wewe ulimwona bibi, mimi n'kamwona kibibi.
Ulipenda, nikapenda, na wala bila kusita
Silaikiwi zaidi kukupita, bwana wangu.
Tua yako ilikuwa kule kwenye masanduku;
Hata yangu kadhalika, mambo yalivyotokea;
Kwani niliposa hapa hata nikatoka jasho,
Na kuapa hadi kichwa changu kikawa kikavu
Kwa viapo vya mapenzi, mwisho—kama ni ahadi—
Nikiahidiwa naye, na kizuri huyu hapa,
Kulipata pendo lake, ikiwa bahati yako
Itampata bibiye.

POSHIA: Hii ni kweli, Nerissa?
NERISSA: Bibie, hivyo ni kweli, basi ufurahi pia.
BASSANIO: Wewe nawe Gratiano, utakuwa mwaminifu?
GRATIANO: Naam, hakika, bwanangu.
BASSANIO: Siku kuu yetu sisi itaheshimika sana
Katika arusi yenu.
GRATIANO: Bali nani huyu aja? Lorenzo na kafiriye?
Hebu, na rafiki yangu wa zamani, Salarino?

(*Aingia Lorenzo, Jessika na Salarino*)

BASSANIO: Lorenzo na Salarino, nyote karibuni hapa;
Kama hadhi yangu mpya inao uwezo hapa
Wa kuwakaribisheni. Kwa ruhusa yako wewe
Poshia mwema, nawakaribisha rafiki zangu,
Na wananchi wenzangu.
POSHIA: Na mimi pia, bwanangu:
Wote wanakaribishwa.
LORENZO: Nashukuru, bwana wangu. Kwangu mimi, bwana wangu,
Haikuwa nia yangu kuja kukuona hapa;
Bali nilipokutana na Salarino njiani,
Alinishawishi sana, nisiweze kukataa
Kuwa nifatane naye.
SALARINO: Ni sawa sawa, bwanangu;
Na siyo bila sababu; Maulana Antonio
Kamtuma kuja kwako. (*Anampa barua*)
BASSANIO: Kabla sijafungua,
Nakusihi nijulishe hali ya rafiki yangu.
SALARINO: Si mgonjwa, bwana wangu, ila labda moyoni;
Na wala siyo mzima, ila labda moyoni:
Na hiyo barua yake 'takuonya hali yake.

(*Bassanio asoma barua*)

GRATIANO: Nerissa, mchangamshe yule mgeni mwingine;
Mwambie akaribishwa.—Mkonowo, Salarino:
Je, Habari za Venisi? Mtukufu Antonio,

Yule tajiri mwanana, yu katika hali gani?
Najua atafurahi kwa huku kufuzu kwetu;
Sisi ni kina Jasoni, tumejipatia sufu.

SALARINO: Heri mngejipatia sufu aliyopoteza.

POSHIA: Kuna habari si njema katika barua ile
Zinazomtoa rangi Bassanio mashavuni:
Kafiwa na rafikiye, ama hapana cho chote
Duniani kingeweza kubadili hivyo hali
Ya mwanamume imara. Lo, yazidi kuwa mbaya!—
Kunradhi, Bassanio; ni nusu yako mwenyewe,
Sina budi nifahamu nusu ya jambo lo lote
Ambalo barua hii imekuja nalo kwako.

BASSANIO: O, Poshia mwema, kuna maneno mabaya hapa
Kupita maneno yote yalopata kuandikwa
Kuchafua karatasi! Bibi mpole, mapema,
Nilipokufunulia moyo wangu wa mapenzi,
Nilisema wazi wazi kuwa mali yangu yote
Ni damu yangu mwilini,—nilipata kuwa mtu;
Kisha nikasema kweli: Lakini, bibi mpenzi,
Japo sikujisifia, utaona jinsi gani,
Ambavyo nilijigamba. Nilipokwambia kuwa
Hali yangu si cho chote, ingefaa nikwambie
Kuwa ni mbaya zaidi; kwani ukweli ni kuwa
Nimekula fadhiliye rafiki yangu mpenzi,
Na yeye kala fadhili ya mtu adui yake
Ili anitimizie. Barua ni hii, bibi.
Karatasi ni sawa na mwili wa sahibu yangu,
Na kila neno la humo ni kama jeraha wazi
Ambalo latoka damu. Walakini, Salarino?
Nambie, hivi ni kweli? Biashara zake zote?
Hakupata hata moja? Ya kutoka Tripoli,
Ya kutoka Mexico, kutoka Uingereza,
Liziboni, Baribari, na kutoka Bara Hindi?
Hata merikebu moja haikuwahi kuponywa,

Na miamba mifishaji ya wafanya biashara?
SALARINO: Hata moja, bwana wangu; pia inaelekea
Kuwa japo angekuwa ana fedha za kulipa,
Yahudi angekataa. Sijapata kumjua
Kiumbe sawa na huyo, mwenye sura kama mtu,
Mwenye nia na tamaa ya kumwangamiza mtu.
Anamwudhi Sultani asubuhi na usiku;
Tena anaukashifu hata uhuru wa nchi,
Kama akinyimwa haki: matajiri ishirini,
Na Sultani mwenyewe, na mamwinyi wa mjini
Wenye taadhima kubwa, wote wamemnasihi:
Bali hapana mmoja aloweza kumwachisha
Dai lake la husuda, ambalo kang'ang'ania,
La kutaka malipizi, haki na shahada yake.
JESSIKA: Nilipokuwa ninaye 'limsikia kuapa
Kwa Tubali na kwa Chusi, watu wa kabila lake,
Kwamba heri achukue nyama yake Antonio,
Kulikoni fedha zake hata mara ishirini,
Ya zile anazomwia: na, najua, bwana wangu,
Kwamba sheria, amri, na enzi visipopinga,
Maskini Antonio atatiwa taabuni.
POSHIA: Ni rafikiyo mpenzi aliye hivi ta'buni?
BASSANIO: Rafiki kipenzi kwangu, mtu mwema wa ajabu,
Mwelekevu na mpole, ambaye kamwe hachoki
Katika kutenda mema; mtu mmoja ambaye
Kajaziwa utukufu wa Roma ya kizamani
Kuliko mtu ye yote aishiye Italia.
POSHIA: Anawiwa na Yahudi deni la kiasi gani?
BASSANIO: Kwa ajili yangu mimi, dukati elfu tatu.
POSHIA: Hizo basi, si zaidi?
Mlipe elfu sita na kuifuta shahada;
Vikwi sita maradufu, na halafu mara tatu,
Kabla mtu rafiki mwenye sifa kama hiyo
Hajapoteza unywele kwa kosa la Bassanio.

Kwanza twende kanisani, uniite mke wako,
Kisha uende Venisi kwa huyo rafiki yako.
Kwani kamwe hutalala pamoja naye Poshia
Una fadhaa moyoni. Utakuwa na dhahabu
Kulipa hicho kideni zidi mara ishirini:
Likisha lipwa, mlete rafiki yako mkweli.
Na katika muda huo, mimi na Nerissa wangu,
Tutaishi kama wali na wajane. Haya, twende!
Kwani utatoka hapa siku ya arusi yako:
Wakaribishe rafiki, onyesha kichangamko:
Umenunuliwa ghali, nitakupenda kwa moyo.
Hebu kwanza nisikie barua ya rafiki yako.

BASSANIO: (*anasoma*)

'Bassanio mwema, meli zangu zote zimepotea, wadai wangu wanazidi ukatili, hali yangu iko chini sana, shahada yangu kwa Yahudi imebatilika; na kwa kuwa baada ya kuilipa haiwezekani nibaki hai, nitakuwa sikudai kitu cho chote, ikiwa nitaweza angalau kukuona tu kabla sijafa. Lakini pamoja na hayo usijikalifu: kama pendo lako halitakufanya uje, barua yangu isikushawishi.'

POSHIA: O, mpenzi, harakisha shughuli zote, uende!

BASSANIO: Madhali kwa wema wako, nina ruhusa ya kwenda,
Nitaondoka haraka: bali, pindi nirudipo,
Kamwe sitajinyoosha kwenye cho chote kitanda,
Raha haitatutenga sisi wawili tulipo.

(*Wanatoka*)

III . 3

Venisi. Barabarani

(*Aingia Shailoki, Salanio, Antonio na Mlinzi-Jela*)

SHAILOKI: Askari, mwangalie: usinambie huruma;
Huyu ndiye mpumbavu alotoa fedha bure:
Askari, mwangalie.
ANTONIO: Hebu unisikilize kwanza, Shailoki mwema.
SHAILOKI: Nataka shahada yangu; 'sipinge shahada yangu;
Nimesha kula kiapo nipate shahada yangu.
Wewe ulinita mbwa bila kuwa na sababu;
Bali, madhali ni mbwa, angalia meno yangu;
Sultani hana budi atanipa haki yangu.
Ajabu, mlinzi mbaya, kwamba unapenda sana,
Kutoka nje pamoja naye kama aombavyo.
ANTONIO: Nakusihi, tafadhali, unisikie niseme.
SHAILOKI: Nataka shahada yangu; sikusikii useme;
Nataka shahada yangu; basi usiseme tena.
Sitakubali kubembwa na kufanywa mpumbavu,
N'tikise kichwa, nipoe, nipumue, nikubali,
Ya wasihi Masihiya. 'Sinifuatefuate;
Sitaki kusemasema: nataka shahada yangu.
(*Anatoka*)
SALANIO: Hili ndilo jibwa gumu kupita majibwa yote
Yaliyoishi na watu.
ANTONIO: Basi, mwachilie mbali:
'Sizidi kumfuata na maombi yasofaa.
Ataka maisha yangu; kisa chake nakijua:
Mara nyingi niliponya katika adhabu zake
Wengi walokuja kwangu mara na mara kulia:
Kwa hiyo anichukia.
SALANIO: Bila shaka Sultani
Hatakubali kabisa adhabu hii ilipwe.

ANTONIO: Sultani siyo mweza wa kuipinga sheria:
Maana walicho nacho wageni pamoja nasi
Katika mji Venisi, wao wakihiniwacho,
Sheria ya mji huu itatiwa mashakani;
Biashara na faida ya mji huu hupatwa
Toka mataifa yote. Kwa hiyo, basi enenda:
Nimedhoofishwa mno kwa huzuni na hasara,
Hata sifahamu kesho nitavyoweza kumpa
Mdai wangu katili hiyo ratili ya nyama.
Enenda zako, mlinzi. Omba Mungu Bassanio
Aje aone mwenyewe nikilipa deni lake,
Halafu sijali kitu!

(*Wanatoka*)

III . 4

Belimonti. Chumba, nyumbani kwa Poshia

(*Aingia Poshia, Nerissa, Lorenzo, Jessika na Baltazari*)

LORENZO: Bibie, japo nasema na wewe mwenyewe upo,
Jinsi yako ya kujua urafiki wa kimungu,
Ni tukufu na halisi, ambayo yadhihirika
Vile uvumiliavyo kutokuwepo bwanao.
Lakini ungemjua, umheshimuye hivi,
Jinsi alivyo mwungwana, uliyempa faraja,
Alivyo sahibu tunu, wa bwana wangu mumeo,
Najua ungejivuna zaidi kwa tendo hili,
Kuliko unavyopaswa kwa wema wa kawaida.
POSHIA: Sijajuta asilani kwa kutenda jambo jema,
Wala sitajuta sasa: kwani baina ya wenzi
Waongeao pamoja na kupitisha wakati,
Wachukuao nyoyoni kima sawa cha mapenzi,
Hapana budi pawepo kiasi kingine sawa
Cha umbile, cha tabia, na cha hali ya mtima;

Inifanyayo kuwaza, kuwa huyu Antonio,
Alo sahibu mpenzi wa moyo wa bwana wangu,
Hana budi afanane na bwanangu. Kama ndivyo,
Gharama ni duni sana, ambayo nimeilipa,
Ili kumgharimia, kifani cha roho yangu,
Kumkomboa katika ukatili wa kinyama!
Haya yafanana mno na kujisifu mwenyewe;
Basi, yasisemwe tena. Sikia mambo mengine.
Lorenzo, nakukabidhi katika mikono yako,
Ulinzi wa nyumba yangu na usimamizi wake
Hadi bwanangu arudi: mimi kwa upande wangu,
Nimeiapia mbingu, kiapo cha siri kwamba,
Nitaishi kwa kusali pia kwa kutafakari,
Huku nikitumikiwa na Nerissa peke yake,
Hadi hapo mume wake na bwanangu warudipo:
Kuna nyumba ya watawa yapata maili mbili;
Ndipo nitakapoishi. Naomba usikatae
Wajibu huu ambao pendo langu na dharura
Vyakufanya kuchukua.

LORENZO: Kwa mtima wangu wote;
Bibi, nitakutii kwa amri zote za haki.

POSHIA: Watu wangu wafahamu tayari mawazo yangu,
Nao watakukubali wewe pamwe na Jessika,
Badala ya Maulana Bassanio pamwe nami.
Na sasa, basi, kwa heri, hadi tutapoonana.

LORENZO: Mawazo mema na saa za furaha viwe nawe!

JESSIKA: Nakutakia bibie, kila ridhaa ya moyo.

POSHIA: Nakushukuru kwa ombi lako, nami nafurahi
Kukwombea vivyo hivyo: haya kwa heri, Jessika.

(*Jessika na Lorenzo wanatoka*)

Sasa basi, Baltazari, kama nilivyokujua,
Mkweli na mwaminifu, ningependa hata sasa
Uwe ukingali hivyo. Chukua barua hii,

Ufanye kila juhudi awezayo mwanamume
Kufika hima Padua: mkabidhi mkononi,
Binamu yangu mwenyewe, Daktari Bellario;
Ona maandiko gani na mavazi atakupa,
Uyalete, nakusihi, kwa haraka uwezavyo,
Hadi kule kivukoni, kiungacho na Venisi.
Usipoteze wakati katika kusemasema,
Bali enenda upesi: 'tanikuta kivukoni.

BALTAZARI: Bibie, nakwenda kasi, kadiri itakiwavyo.

(*Anatoka*)

POSHIA: Haya nifate, Nerissa; nakusudia shughuli
Ambayo hujaijua; tutaona bwana zetu,
Wao hawajatuwaza.

NERISSA: Je, nao watatuona?

POSHIA: Watatuona, Nerissa; lakini katika vazi
Litofanya watudhani tunacho tusicho nacho.
Niko tayari tupinge nikupe kitu cho chote,
Wawili tutapovaa kujifanya wavulana,
Baina yetu wawili nitapendeza zaidi,
Na kujifunga jambia likashamiri zaidi;
Na kusema kwa sauti inokwaruzakwaruza,
Ilivyo ya kivulana; na hatua mbili fupi,
Nitazichanganya ziwe moja ndefu ya kiume;
Nitajigamba magomvi, kwa makeke ya ujana;
Na kusema wongo mwingi, jinsi gani nilipendwa,
Na mabibi wa heshima, nami nikawakataa,
Wakaugua wakafa; wala mimi sikujali;
Na halafu nikajuta, na kusema baadaye,
Kwamba ingekuwa bora, kama nisingewaua:
Na uwongo kama huu nitasema ishirini;
Hata watu watasema, kuwa nimeacha shule
Zaidi ya mwaka moja: nina elfu kichwani,
Hila hizi za kitoto za hawa wanojigamba,
Nitakazojizoeza. Walakini twende zetu,

Nitakwambia mzima mpango nilio nao
Hapo nitakapokuwa ni ndani ya gari langu,
Ambalo latusubiri langoni mwa bustani;
Kwa hiyo twende upesi, kwani mwendo wetu leo
Ni maili ishirini.

(*Wanatoka*)

III . 5

Belimonti. Bustanini

(*Aingia Launseloti na Jessika*)

LAUNSELOTI: Naam, hakika, kwani, sikia, dhambi za baba hulipwa na watoto: kwa hiyo, nakwambia nakuhofia. Daima nimekwambia kweli, na kwa hiyo sasa nakwambia mawazo yangu juu ya jambo hili; kwani, hakika, nadhani umeangamia.

JESSIKA: Nitaponywa na mume wangu; amenifanya Mkristo.

LAUNSELOTI: Hakika, hiyo inakuzidishia lawama; tulikuwa na Wakristo wa kutosha kabla yako; wengi kadiri ilivyowezekana kusaidiana. Huku kuzidisha Wakristo kutaongeza bei ya nguruwe; ikiwa wote tutaanza kuwa walaji wa kamsengere punde tutashindwa kupata chembe ndogo ya nguruwe japo makaa yawe fedha.

JESSIKA: Nitamwambia mume wangu usemavyo, Launseloti: Ni huyu anakuja.

(*Aingia Lorenzo*)

LORENZO: Karibu nitaanza kukuonea wivu, Launseloti, ikiwa utakuwa unamwingiza hivyo mke wangu pembenipembeni.

JESSIKA: La, usiwe na hofu juu yetu, Lorenzo: Launseloti nami tumegombana. Ananambia wazi kabisa kwamba sitapata rehema mbinguni, kwa sababu ni binti wa

Yahudi: na anasema, wewe si mwananchi mwema, maana kwa kuwafanya Mayahudi wawe Wakristo, unapandisha bei ya nguruwe.

LORENZO: (*kwa Launseloti*) Nenda ndani, fidhuli we; waambie wajitayarishe kwa chakula.

LAUNSELOTI: Wameshajitayarisha, bwana; wote wana matumbo.

LORENZO: Mungu wangu, u mwepesi sana wa kujibu! Basi kawaambie watayarishe chakula.

LAUNSELOTI: Hilo pia ni tayari, bwana, ila neno ni andiko.

LORENZO: Kaandike, basi, bwana!

LAUNSELOTI: Wala siyo hivyo, bwana; najua wajibu wangu.

LORENZO: Ugomvi zaidi kila wakati! Utaonyesha uhodari wako wote mara? Tafadhali; mwelewe mtu wa kawaida kwa maana ya kawaida; nenda ndani kwa wenzako, wambie waandike meza; waandae na chakula, nasi tutakuja kula.

LAUNSELOTI: Meza, bwana, itaandikwa; chakula, bwana, kitaandaliwa; na tena, basi, vicheko na utani vitatawala.

(*Anatoka*)

LORENZO: Hana tanadhari hata, apachika tu maneno!
Juha kapanda kichwani jeshi la maneno mema!
Nami nawajua wengi, walio na hali bora,
Wengi wa maneno vivyo, wayatumiayo ovyo.
U hali gani, Jessika? Na sasa, kizuri mwema,
Nambie mawazo yako, jinsi unavyompenda,
Mkewe Bwana Bassanio.

JESSIKA: Wala sina la kusema. Itakuwa vema sana
Kama Bwana Bassanio ataishi bila doa;
Maana kwa kujaliwa kumpata bibi huyu,
Aipata duniani mibaraka ya peponi.
Na asipostahili hii hapa duniani,
Atakuwa hana haki ya kuingia peponi.
Kwani miungu wawili wangeamua kucheza

Kamari ya kipeponi, walipane wanawake
Wawili wa kidunia, na Poshia mmojapo,
Lazima wa pili wake awe ni kitu kingine
Maana dunia nzima haina kifani chake.

LORENZO: Kumpata mume mimi una baraka ya mume
Alivyo baraka ya mke.

JESSIKA: Hayo niulize mimi.

LORENZO: Nitakuuliza punde: lakini kwanza tukale.

JESSIKA: Siyo, nikusifu kwanza nikingali na shauku.

LORENZO: Laa nakusihi, hayo yawe soga za mezani;
Hapo ungasema nini nitaweza kulimeza,
Pamwe na vitu vingine.

JESSIKA: Vizuri, nitakusifu.

(*Wanatoka*)

IV · 1

Venisi. Katika Mahakama

(*Aingia Mtawala, Msafara wa Mamwinyi, Antonio, Bassanio, Gratiano, Salarino na Wengineo*)

SULTANI: Je, Antonio yu hapa?
ANTONIO: Ni tayari, muadhamu.
SULTANI: Nakuhurumia sana: umekuja kumjibu
Mtu jiwe na jahili, mwenye roho ya kinyama,
Asokuwa na huruma, wala tone la rehema.
ANTONIO: Nimesikia mwadhamu, kwamba umejitahidi
Kumuomba alegeze nia alodhamiria;
Na kwa kuwa kakaidi, wala hakuna sheria
Kunifanya niepuke kucha za kisasi chake,
Basi nitapambanisha ghadhabuye kwa subira,
Ni tayari kuhimili kwa moyo wa utulivu
Ujahili wake wote na vishindo na ghadhabu.
SULTANI: Ende mtu amlete Yahudi mahakamani.
SALARINO: Yu tayari mlangoni: anakuja, bwana wangu.
(*Shailoki anaingia*)
SULTANI: Hebu fanyeni nafasi, asimame mbele yangu.
Shailoki, ulimwengu hata mimi vile vile,
Twadhani wang'ang'ania njia hii ya kisasi
Hadi ufikie mwisho; halafu inadhaniwa
Utaonyesha rehema na majuto ya ajabu
Kuzidi ukatiliwo uonekanavyo sasa;
Na kwamba ijapokuwa sasa wadai malipo,
Ratili moja ya nyama, ya mwili wa maskini
Mfanya biashara huyu, hutaisamehe tu,
Bali kwa kushikwa pendo na upole wa kiutu

Pia utamsamehe nusu ya rasilimali.
Tupa jicho la huruma uzitazame hasara
Zilizomuelemea siku hizi za karibu,
Za kutosha kumwangusha tajiri mkubwa sana
Na kuifanya haliye ikakamua huruma
Toka vifua vya shaba, myoyo migumu ya mawe,
Kwa Maturuki kaidi hata kwa Mataritari
Wasopata kufundishwa jamala na uungwana.
Wote tunatazamia jibu amana, Yahudi.

SHAILOKI: Nimekweleza, mwadhamu, nini nimedhamiria,
Na kwayo sabato yetu takatifu nimeapa,
Kwamba nitalipwa haki na haka ya hati yangu:
Na kama ukinihini basi na iangamie
Katiba ya mji wenu pamwe na uhuru wake.
Mtauliza kwa nini nachagua kupokea
Ratili moja ya nyama ya kuoza na kuvunda,
Badala ya kuchukua dukati elfu tatu:
Na mimi nitakataa kulijibu swali hilo;
Bali niseme ya kwamba, napenda tu: nimejibu?
Nikijiona nyumbani nasumbuliwa na panya,
Nikapendezwa kutoa dukati elfu kumi
Ili kumuangamiza! Je, bado sijakujibu?
Wako watu wasopenda nguruwe aachamaye:
Wengine huwa kichaa kama wakimwona paka;
Na tena kuna wengine wakisika zumari
Kamwe hawatulizani: kwani shauku ya moyo,
Bibie harara kuu, huuongoza mtima
Kupenda na kuchukia. Na sasa nitakujibu:
Kama hakuna sababu inoweza kutolewa
Kwa nini huyu hapendi nguruwe aachamaye;
Kwa nini yule hapendi paka asiye na dhara;
Huyu zumari ya sufu; lakini inambidi
Kwa kuwa ameudhiwa, na yeye pia audhi;
Kwa hiyo sina sababu, wala sitoi sababu,

Ila kwamba nina chuki, na kwamba namkirihi
Mtu huyu Antonio, kwa hiyo nang'ang'ania
Mashtaka haya kwake. Je, sasa umejibika?

BASSANIO: Jibu hilo siyo jibu, wewe kiumbe jahili,
Kwamba liwe ni sababu ya kufanya ukatili.

SHAILOKI: Silazimiki kutoa jibu la kukupendeza.

BASSANIO: Watu wote huviua vitu wasivyovipenda?

SHAILOKI: Yuko anayechukia asotaka kukiua?

BASSANIO: Awalini kila kosa halianzi kama chuki.

SHAILOKI: Wewe ungependa nyoka akuume mara mbili?

ANTONIO: Nakusihi ukumbuke, unamhoji Yahudi:
Afadhali ungekwenda usimame huko pwani
Uombe maji makuu kupunguza nguvu zake;
Na tena ni afadhali kumhoji mbwa mwitu
Kwa kumfanya kondoo amlilie mwanae;
Heri na misonobari milimani uiase
Isitikise vilele wala kufanya kelele
Wakati inaposongwa na dhoruba za mbinguni;
Afadhali kujaribu jambo gumu la magumu
Kuliko kulainisha kisozidiwa ugumu—
Moyo wa Yahudi huyu: kwa hiyo ninakusihi,
'Simpe cho chote tena,' simshawishi zaidi,
Ila bila kuchelewa na inavyostahili,
Acheni nihukumiwe, na Yahudi aridhike.

BASSANIO: Kwa dukati tatu elfu, twaa hizi sita elfu.

SHAILOKI: Ijapo kila dukati, katika elfu sita,
Iwe na vipande sita, kila kimoja dukati,
Nisingalizipokea; naitaka haki yangu.

SULTANI: Utapataje rehema, usojua kurehemu?

SHAILOKI: Nihofu hukumu gani, mimi nisiye na kosa?
Nyinyi wenyewe mnao waja wa kununuliwa,
Ambao kama vihongwe na mbwa na nyumbu wenu,
Mwawatumia katika shughuli duni za kija
Kwani mliwanunua: naweza kuwambieni,

Wacheni waende huru, waozwe warithi wenu?
Mbona wanahangaika? Acheni vitanda vyao
Viwe safi kama vyenu, na vinywa vyao vionje
Vinono mnavyovila? Najua mtanijibu,
Watumwa hao ni wetu: nami nawajibu vivyo:
Ratili moja ya nyama, ambayo ninamdai
Imelipiwa aghali; ni yangu, na naitaka.
Kama mkiininyima, kefule sheria zenu!
Hazina nguvu yo yote sheria za mji huu.
Mimi nadai hukumu: jibuni, nitaipata?

SULTANI: Kwa nguvu zangu naweza kuvunja baraza hili,
Ila kama Bellario, mwanasheria hodari,
Ambaye nimemwagiza kuja kutoa shauri,
Atafika leo hii.

SALARINO: Bwana wangu, hapa nje
Amewasili mjumbe anayetoka Padua,
Naye kaja na barua za huyo mwanasheria.

SULTANI: Zilete hizo barua; kamwite huyo mjumbe.

BASSANIO: Changamka, Antonio! Piga moyo konde bado!
Yahudi atachukua mwili wangu, damu yangu,
Mifupa na kila kitu, kabla ya tone moja
La damuyo kutolewa kwa ajili yangu mimi.

ANTONIO: Kwenye kundi la kondoo maksai wa mawaa
Kifo ni wajibu wake: na tunda bovu la yote
Ni la kwanza kuanguka; nami niacheni vivyo:
Huwezi kufanya kazi ilo bora Bassanio,
Kuliko kubaki hai unitungie ubeti
Juu ya kaburi langu.

(*Aingia Nerissa, kavaa kama karani wa wakili.*)

SULTANI: Umetokea Padua, kutoka kwa Bellario?

NERISSA: Naam, bwana wangu, Bellario akusalimu.

(*Anatoa barua*)

BASSANIO: Kwa nini umekazana kukinoa kisu chako?

SHAILOKI: Ili nikate mnofu kwa mfilisika yule.

GRATIANO: Hukinolei wayoni, wakinolea moyoni
Ewe Yahudi katili; bali hakuna madini,
Hata shoka la mnyonga, liwezalo kuwa kali
Nusu ya kisasi chako. Hata huchomwi kwa sala?
SHAILOKI: La, sala hainichomi, yo yote utayobuni.
GRATIANO: O, ulaanike, ewe jibwa lisilo huruma!
Na haki ishitakiwe kukuachia uzima.
Karibu unanifanya nishuku imani yangu
Na kuanza kuamini kama Paithagorasi,
Kwamba roho za wanyama pengine hujiingiza
Kwenye miili ya watu: roho yako ya kijibwa
'Litawala mbwa mwitu alomwua binadamu,
Na wakati wa kunyongwa ilikimbia haraka,
Ikakuta umelala tumboni mwa mama yako,
Ikakaa ndani yako; maana tamaa zako
Ni za kimbwa wa mwitu, za damu, njaa, ulafi.
SHAILOKI: Bila kuwa na uwezo wa kukemea muhuri
Ubanduke uondoke katika shahada yangu,
Bure unayaumiza mapafu yako mwenyewe,
Kwa hizo kelele zako: zitunze akili zako,
Ewe mvulana mwema, ama zitaharibika
Zisiweze kuponyeka. Nangojelea sheria.
SULTANI: Barua ya Bellario yampendekeza kwetu
Kijana mtaalamu, daktari wa sheria.
Yu wapi kijana huyo?
NERISSA: Yu karibu asubiri,
Alijue jibu lenu, kama mtamkubali.
SULTANI: Kwa mtima wangu wote. Enendeni kati yenu,
Watatu au wanne mumlete kwa heshima.
Na tunapokisubiri baraza litasikia
Barua ya Bellario.

KARANI: (*anasoma*) Muadhamu ufahamu, kwamba nilipopokea barua yako nilikuwa mgonjwa sana: lakini wakati ule ule nilipoipata barua yako ikawa ninaye mgeni

mpenzi, kijana mtaalam kutoka Roma; jina lake Baltazari. Nilimweleza kisa cha mashtaka baina ya Yahudi na mfanya biashara Antonio: tulifunuafunua vitabu vingi pamoja: na nimemweleza maoni yangu; ambayo, kwa kusaidiwa na utaalam wake mwenyewe, ambao ni mkubwa kiasi nisichoweza kusifia vya kutosha, nimemwomba aje nayo, ili atimize maombi yako, mwadhamu, badala yangu. Nakusihi sana, ujana wake usifanye apunguziwe heshima; kwani sijapata kuona mwili kijana wenye kichwa kilichopevuka kama cha kijana huyu. Namkabidhi mikononi mwa utukufu wako, ambamo mashtaka hayo yataeneza sifa zake.

SULTANI: Mwasikia mtaalamu Bellario asemavyo:
Na daktari, nadhani, ni huyu anoingia.
(*Aingia Poshia, amevaa kama daktari wa sheria*)
SULTANI: Unipe mkono wako. Watoka kwa Bellario?
POSHIA: Sawa sawa, bwana wangu.
SULTANI: Karibu: kaa kitako.
Wafahamu mashitaka yalo hapa barazani.
POSHIA: Nayafahamu vizuri, mashitaka yalo hapa.
Nani mfanya biashara, na nani ni Yahudi?
SULTANI: Antonio na Mzee Shailoki, simameni.
POSHIA: Jina lako Shailoki?
SHAILOKI: Shailoki jina langu.
POSHIA: Mashitaka ufanyayo ni ya ajabu kabisa;
Bali unayaendesha kwa mujibu wa sheria
Na sheria ya Venisi haiwezi kukupinga.
(*Kwa Antonio*)
Wewe uko chini yake, watambua ama sivyo?
ANTONIO: Naam, ndivyo asemavyo.
POSHIA: Waikubali shahada?
ANTONIO: Naikubali.
POSHIA: Basi, Yahudi apaswa, kuwa mtu wa rehema.
SHAILOKI: Nalazimishwa na nini? Hebu niambie hilo.

POSHIA: Si tabia ya rehema kutolewa kwa lazima,
Huanguka kama mvua nyororo kutoka juu,
Ikatonekea chini: ina baraka kuwili;
Hubariki mtoaji, na pia mpokeaji:
Ni nyingi kwa wenye vingi: Humlaiki zaidi
Mfalme mwenye taji kulipita taji lake;
Kirungu chake cha enzi ni cha uwezo wa muda,
Ambao ni fani yake ya fahari na adhama,
Ndiyo asili ya kucha na kuhofu wafalme.
Bali rehema yazidi enzi hii ya kirungu;
Ndiyo yenye enzi kuu nyoyoni mwa watawala.
Ni sifa yake Manani, Mwinyezi Mungu mwenyewe.
Utawala wa dunia hufanana na wa Mungu
Inapokuwa rehema yaikamilisha haki.
Japo unadai haki; fikiri hivi, Yahudi;
Haki ingalitimizwa hapana myongoni mwetu
Wa kuupata wokovu: tuombacho ni rehema;
Basi sala hiyo hiyo inatufundisha sote
Kutekeleza rehema. Nimesema yote haya
Kupunguza dai lako la malipizi ya haki,
Ambayo uking'ang'ana, baraza hili la haki,
Litahukumu kushindwa kwa mfanya biashara.
SHAILOKI: Matendo yangu na yawe ni juu ya kichwa changu!
Ninaisihi sheria inilipe haki yangu—
Adhabu na malipizi kwa mujibu wa shahada.
POSHIA: Kashindwa kulipa fedha?
BASSANIO: Mimi nitamlipia hapa hapa barazani,
Naam, hata maradufu: kama hiyo haitoshi,
Nitalipa mara kumi, na kama nisipoweza,
Achukue kichwa changu, mikono na moyo wangu.
Na hii isipotosha, basi itadhihirika
Uovu wafisha haki; nami nakusihi sana,
Uipokonye sheria, kwa uwezo ulo nao.

Kwa kutenda jema kubwa na utende baya dogo.
Akingwe bilisi huyu kutimiza nia yake.
POSHIA: Hilo haliwezekani; hapana nguvu Venisi
Iwezayo kubadili sheria iliyowekwa;
Itawekwa kumbukumbu, na makosa mengi mengi
Yatafanyika nchini, kwa mfano huo huo:
Katu haiwezekani.
SHAILOKI: Danieli amekuja! Amekuja kuhukumu!
Tena Danieli kweli! Ewe kijana hakimu,
Kijana mwenye busara, O, ninavyokuheshimu!
POSHIA: Tafadhali, hebu nipe shahada niitazame.
SHAILOKI: Hii hapa, muadhamu, shahada yenyewe hii.
POSHIA: Shailoki, umepewa fedha zako mara tatu.
SHAILOKI: Ni nadhiri, ni nadhiri, nina nadhiri mbinguni:
Nitazuri roho yangu? La, ningapewa Venisi.
POSHIA: Ni kweli shahada hii haikutimizwa sawa;
Na kufuata sheria, Yahudi huyu aweza,
Kudai ratili moja ya nyama ya mdeniwe,
Ajikatie mwenyewe, karibu sana na moyo,
Wa mfanya biashara. Mfadhili kwa rehema:
Fedha zako mara tatu chukua, uniambie
Nichane shahada hii.
SHAILOKI: Itakapokwisha lipwa kwa shabaha yake hasa.
Inaelekea kuwa u hakimu mwenye haki;
Waifahamu sheria, ulivyoifafanua
Ni fasihi sawa sawa: nakusuta kwa sheria,
Ambayo wewe mwenyewe ni nguzoye stahiki,
Uitamke hukumu: naapa kwa roho yangu,
Ulimi wa binadamu hauna uwezo katu
Wa kunigeuza nia: naitaka haki yangu.
ANTONIO: Kwa mtima wangu wote nayasihi mahakama
Kuitamka hukumu.
POSHIA: Basi ilivyo ni hivi:
Kiweke kifua chako tayari kwa kisu chake.

SHAILOKI: O, hakimu mtukufu! O, kijana muadhamu!
POSHIA: Kwa sababu kwa shabaha na kwa nia ya sheria,
Malipizi ni halali ambayo sasa yabidi,
Kufuata hati hii.
SHAILOKI: Ndivyo, hasa: O, hakimu mwenye busara na haki!
Umepevuka zaidi kuupita uso wako!
POSHIA: Kwa hiyo jitayarishe, funua kifua chako.
SHAILOKI: Naam, kidari chake: ndivyo isemavyo hati:
Ama sivyo isemavyo, e, hakimu mtukufu?
'Karibu na moyo wake': ndiyo maneno yenyewe.
POSHIA: Ndivyo; Je, kuna mizani ya kupimia mnofu?
SHAILOKI: Ninayo hapa tayari.
POSHIA: Tafadhali, Shailoki, weka mganga tayari,
Amwangalie jeraha asitoke damu afe.
SHAILOKI: Hivyo ndivyo isemavyo katika shahada yetu?
POSHIA: Hasha, haisemi hivyo: na nini isiposema?
Litakuwa jambo zuri ukitenda kwa huruma.
SHAILOKI: Siioni asilani; haimo kwenye shahada.
POSHIA: Je, mfanya biashara, una jambo la kusema?
ANTONIO: Sina mengi: nimekwisha jishamiri ni tayari—
Ulete mkono wako, Bassanio: buriani!
Usihuzunike kwamba, nimefikwa nayo haya,
Kwa sababu yako wewe; kwani kwa kitendo hiki
Bahati inaonyesha wema mkubwa zaidi
Kuliko kawaidaye: kwani itamwachilia
Binadamu mwovu huyu kuishiwa mali yake,
Na kufika uzeeni fukara mkodoaji
Mwenye uso wa kunyanzi; nami sasa naepushwa
Kitubio cha dawama cha mateso kama hayo.
Nifikishie salaam kwa mkeo mtukufu:
Umsimlie jinsi ya mwisho wa Antonio;
Mwambie nilikupenda, nisifu nikisha kufa;
Na ukisha kumwambia muombe awe hakimu

Kama kweli Bassanio hakupata kupendeka
Usijute kwamba ati utapoteza rafiki;
Naye pia hatajuta alipaye deni lako;
Maana Yahudi huyu akikata ndani sana
N'talilipa papo hapo na kwa moyo wangu wote.

BASSANIO: Antonio, nimeoa mke nimthaminiye
Kama ninavyothamini maisha yangu mwenyewe.
Bali maisha yenyewe, mke wangu na dunia
Havithaminiwi nami kuzidi maisha yako:
Heri nivikose vyote, hata kuvitoa vyote
Kumpa huyu shetani ili nikuponye wewe.

POSHIA: Mkeo asingeweza kukuambia asante,
Angekuwa yu karibu kusikia usemavyo.

GRATIANO:: Nami pia nina mke ambaye ninampenda:
Ni heri angalikuwa yu mbinguni akisihi
Uweza wo wote huko uweze kumgeuza
Hayawani Myahudi.

NERISSA: Vema wasema hayupo;
Ama sivyo ombi hilo lingeichafua nyumba.

SHAILOKI: Ni waume Masihiya! Mimi pia nina binti—
Ni heri mtu ye yote wa ukoo wa Baraba
Angekuwa mume wake kulikoni Masihiya. (*Kando*)
Tunapoteza wakati: nasihi, toa hukumu,

POSHIA: Ratili moja ya nyama ya mfanya biashara,
Ni haki yako, Yahudi. Sheria inaruhusu,
Na hukumu inakupa.

SHAILOKI: E, hakimu mwenye haki!

POSHIA: Na lazima uikate katika kifua chake:
Sheria inaruhusu, na baraza linatoa.

SHAILOKI: O, hakimu mtaali! Hukumu! Jitayarishe!

POSHIA: Subiri kidogo kwanza: kungali jambo jingine.
Hati hii haikupi tone lo lote la damu.
Maneno yasemavyo ni 'ratili moja ya nyama'.
Basi twaa haki yako, hiyo ratili ya nyama;

Ila unapoikata tone moja likitoka
La damu ya Masihiya, ardhi na mali zako,
Kwa sheria ya Venisi, zitatwaliwa na nchi.
GRATIANO: O, hakimu mwenye haki! Haya sikia, Yahudi.
Ni hakimu mtaali!
SHAILOKI: Ndivyo ilivyo sheria?
POSHIA: 'Tajionea mwenyewe sheria inavyosema:
Madhali wataka haki, basi usiwe na shaka,
Kwamba utapata haki kuzidi unavyopenda.
GRATIANO: O, hakimu mtaali! Haya, sikia Yahudi.
Ni hakimu mtaali!
SHAILOKI: Basi nakubali fedha; nilipeni mara tatu,
Na Masihiya aende.
BASSANIO: Na fedha ni hizi hapa.
POSHIA: Ngoja, kwanza! Myahudi atapata haki yote;
Ngoja! Hapana haraka: hatapata ila haki.
GRATIANO: O, Yahudi! Ni hakimu mwenye haki, mtaali!
POSHIA: Kwa hiyo jitayarishe kuikata hiyo nyama,
Bali usimwage damu, wala kukata zaidi,
Au kukata kidogo kuzidi ratili moja:
Endapo utazidisha, au kukata pungufu,
Japo ni kwa chembe ndogo, iwezayo kupunguza,
Au kuifanya nzito, sehemu ya ishirini,
Ya punje moja hafifu, naam, hata mizani,
Ikitisika kama kwa uzito wa unywele—
Huna budi utakufa, na kufilisiwa mali.
GRATIANO: Ni Danieli wa pili, ni Danieli, e Yahudi!
Haya, sasa, we kafiri, sasa umepatikana.
POSHIA: Mbona Yahudi asita? Jitwalie haki yako.
SHAILOKI: Nipeni mtaji wangu mniache nende zangu.
BASSANIO: Nimekwekea tayari; ni huu hapa, pokea.
POSHIA: Amekwisha ukataa hadharani barazani:
Atapata haki tupu na hayo malipo yake.
GRATIANO: Ni Danieli, narudia, huyu Danieli wa pili!

Nakushukuru, Yahudi, kunifunza neno lilo.
SHAILOKI: Siwezi kupata japo mtaji wangu mtupu?
POSHIA: Hupati kitu cho chote ila hiyo haki yako,
Uikate vivyo hivyo kwa hatariyo, Yahudi.
SHAILOKI: Basi kama hivyo ndivyo shetani ambariki!
Nami sitajibu tena swali lo lote zaidi.
POSHIA: Subiri kwanza, Yahudi: hujaachwa na sheria.
Ni mojapo ya sheria za mji huu Venisi,
Kama ikithibitishwa kwamba mgeni ye yote,
Amejaribu kwa hila za dhahiri au siri,
Kumuua mwananchi, raia wa mji huu,
Basi yule alotaka kutendewa tendo hilo,
Ana haki kuchukua nusu nzima ya maliye
Alotaka kumtenda, na ile nusu nyingine
Hutwaliwa na Taifa. Na maisha ya mkosa
Anoweza kuyaponya ni Sultani pekee.
Na wewe sasa, nasema, umo humo mashakani;
Kwani inaonekana kwa vitendo vya dhahiri,
Kwamba kwa njia za wazi na njia za sirisiri,
Umefanya jitihada kuyahasiri maisha
Ya huyu mshtakiwa; basi kwa kitendo hicho
Umejistahilisha adhabu niloitaja:
Mwangukie Sultani, basi, umwombe rehema.
GRATIANO: Omba upewe ruhusa ukajinyonge mwenyewe:
Bali kwa kuwa maliyo imekuwa ya Taifa
Sasa huna japo kamba ya kwenda kujinyongea;
Na kwa hiyo utanyongwa kwa gharama ya Taifa.
SULTANI: Ili kusudi uone tofauti kati yetu,
Narehemu maishayo kabla hujayaomba:
Kwani nusu ya maliyo ni mali ya Antonio;
Na ile nusu ya pili imekuwa ya Taifa,
Nawe ukinyenyekea itafanywa ni faini.
POSHIA: Nakubali, kwa Taifa, ila si kwa Antonio.
SHAILOKI: La, twaeni kila kitu; msinachie maisha;

Mmetwaa nyumba yangu mkitwaa nguzo yake
Ile inoihimili: mmetwaa na maisha
Iwapo mkikitwaa kinachonipa maisha.

POSHIA: Jambo gani Antonio, waweza kumrehemu?

GRATIANO: Apewe kitanzi bure; wallahi 'simpe zaidi.

ANTONIO: Akipenda mtukufu Sultani na baraza
Kumsamehe faini ya nusu ya mali yake,
Mimi nitakuwa radhi; basi ataniachia
Niitumie nyingine; halafu akisha kufa
Nimwachieyo jamaa alotwaa binti yake.
Walakini ni lazima afanye mambo mawili.
La awali sasa hivi akubali kubatizwa;
Na la pili aandike papa hapa barazani,
Kwamba atakapokufa chochote alichonacho
Atamwachia mkwewe, Lorenzo, na binti yake.

SULTANI: Ni lazima akubali haya yote ama sivyo,
Nitakana msamaha nilokwisha kutamka.

POSHIA: Umeridhika, Yahudi? Una jambo la kusema?

SHAILOKI: Ni radhi.

POSHIA: Katibu, itayarishe hati ya maafikano.

SHAILOKI: Tafadhali nawaomba, nachieni niondoke;
Najisikia vibaya: hiyo hati niletewe,
Nami nitaisaini.

SULTANI: Nenda zako, walakini usikose kutimiza.

GRATIANO: Na utakapobatizwa uwe na baba wawili:
Ningalikuwa hakimu, ungeongezewa kumi,
Wakulete kinyongoni, siyo pa kubatiziwa.

(*Shailoki anaondoka*)

SULTANI: Bwana, karibu nyumbani, kwa chakula cha jioni

POSHIA: Nakusihi kwa upole, Mwadhamu, niwie radhi:
Usiku wa leo huu sina budi niondoke
Kuelekea Padua, na bora nianze mara.

SULTANI: Nasikitika ya kwamba huna wasaa mzuri.—
Sikiliza, Antonio, mtuze mwungwana huyu;

Kwani kwa mawazo yangu amekufadhili sana.
(*Sultani anaondoka*)
BASSANIO: Mtukufu muungwana, mimi na rafiki yangu
Kwa busara yako kubwa tumeponywa leo hii
Na adhabu kubwa sana; kwa hiyo tunakusihi,
Dukati elfu tatu, alizodai Yahudi
Tafadhali zipokee zifidie tabu zako.
ANTONIO: Na juu ya hayo yote tuna deni kubwa kwako
La mapenzi na huduma lisilokwisha daima.
POSHIA: Amelipwa vya kutosha alokwisha kuridhika;
Na mimi kwa kukuponya nimekwisha kuridhika,
Na kwa hiyo najiona kwamba nimekwisha lipwa:
Nami kamwe sijapata kupenda fedha zaidi
Nakuomba, unijue tutapokutana tena.
Nakutakia baraka, na sasa nawaageni.
BASSANIO: Mpenzi bwana, sina budi ya kukusihi zaidi:
Twaa kwetu kumbukumbu, iwe kama sifa njema,
Siyo kama ni malipo: naomba mambo mawili.
Kwanza, sinikatalie, na pili niwie radhi.
POSHIA; Wanishurutisha sana, kwa hiyo ninakubali.
(*Kwa Antonio*) Nipe mashikia yako; nami ntakuvaliayo;
(*Kwa Bassanio*) Nawe kwa mapenzi yako, nitatwaa pete hii
Usirudishe mkono, sitachukua zaidi,
Nawe kwa mapenzi yako, hutanihiniyo hii!
BASSANIO: Pete hii, bwana mwema, ni kitu cha duni sana
Na sitajiaibisha kwa kukupa kitu duni!
POSHIA: Kitu kingine sitwai, ila pete hii hii,
Nami sasa nafikiri naipenda pete hii.
BASSANIO: Ina maana zaidi kuliko thamani yake,—
Nitakupa pete bora kupita zote Venisi,
Nako kuipata kwake niipate kwa tangazo:
Lakini kwa pete hii, tafadhali, kunradhi!
POSHIA: Sasa nakuona bwana, u mkarimu maneno:
Wewe mwenyewe awali umenifunza kuomba;

Na sasa unanifunza ajibiwavyo mwombaji.
BASSANIO: Bwana mwema, pete hii alinipa mke wangu;
Na alipokinivisha alinitaka nadhiri,
Nisiuze, nìsitoe, wala nisiipoteze.
POSHIA: Hicho ni kisingizio cha waume wengi sana,
Kuponya zawadi zao. Lakini kama mkeo
Si mwanamke kichaa, na kama akifahamu
Ninavyoistahili pete hii naamini
Hatafanya uhasama utaodumu daima,
Kwa kunipa pete hii. Haya vyema, kwa herini!
(*Poshia na Nerissa wanatoka*)
ANTONIO: Bwana wangu Bassanio, mwachie atwae pete:
Acha stahiki yake pamwe na mapenzi yangu
Vilingane na thamani ya amri ya mkeo.
BASSANIO: Enenda, Gratiano, kimbia umfikie;
Umpeyo pete hii; na kama yawezekana,
Mlete kwa Antonio. Ondoka! Enenda hima.
(*Gratiano anaondoka*)
Njoo, sisi yatupasa kuondoka mara moja;
Na asubuhi ya kesho mapema mimi na wewe
Tutakwenda Belimonti: twende zetu, Antonio.
(*Wanaondoka*)

IV · 2

Venisi: Barabarani

(*Aingia Poshia na Nerissa wamevaa kama mwanzo*)

POSHIA: Katafute kwa Yahudi na kumpa hati hii,
Ili atie sahihi; kisha rudi twende zetu.
Lazima twondoke leo, ili tuwahi nyumbani
Siku moja kabla ya waume zetu kurudi.
Atafurahika sana Lorenzo kwa hati hii.
(*Aingia Gratiano*)

GRATIANO: Bwana mwema, nimefika kwako na habari njema,
Bwana wangu Bassanio, kanasihika zaidi,
Akanipa pete hii nije nikuleteeyo;
Tena akukaribisha kwa chakula cha jioni.
POSHIA: Hiyo haiwezekani: pete yake napokea,
Kwa wingi wa shukurani: na ndivyo nikuombavyo,
Umwambie arudipo: vile vile nakuomba,
Mwonyeshe kijana wangu nyumbani kwa Shailoki.
GRATIANO: Hilo nitalitimiza.
NERISSA: Bwana, napenda tuseme.
(*Kando kwa Poshia*) Nitajaribu kupata pete yake mume wangu;
Ambayo nilimwapisha aishi nayo daima.
POSHIA: *Kando kwa Nerissa*) Nadhani utaipata. Kisha wataapa sana
Ya kwamba pete zenyewe wamewapa wanaume;
Lakini tutawashinda na tutaapa zaidi.
(*Kwa sauti*) Haya! enenda haraka wajua n'takosubiri.
NERISSA: Njoo, bwana mwema, utanionyesha nyumba hiyo?
(*Wanaondoka*)

V . 1

Belimonti. Barabara iendayo nyumbani kwa Poshia

(*Aingia Lorenzo na Jessika*)

LORENZO: Mbaamwezi inang'aa: ni usiku kama huu,
Ule upepo mwanana ulipoibusu miti,
Kwa upole na utuvu, na miti ikatulia,
Ni usiku kama huu, nadhani Troilusi
Alipanda kuta zile zilozingia Troi,
Na moyowe kuhemea mahema ya Magiriki,
Ambako usiku ule Kiressida alilala.
JESSIKA: Ni usiku kama huu, ndipo Thisibe kwa woga,
Alinyata umandeni, akakiona kivuli,
Cha simba ki mbele yake, akakimbia kwa hofu.
LORENZO: Ni usiku kama huu, Dido aliima pwani,
Kwenye kingo chafu sana, mkambezo mkononi,
Kupungia mpenziye arejee Karthago.
JESSIKA: Ni usiku kama huu, Medea alikusanya
Mitishamba ya uchawi, ilorudisha ujana,
Kwa mzee Aesoni.
LORENZO: Ni usiku kama huu, Jessika alitoroka
Kwa Yahudi mwenye mali, na kwa pendo lisofaa,
Akakimbia Venisi, akaenda Belimonti.
JESSIKA: Ni usiku kama huu, ndipo kijana Lorenzo
Alipomwapia kuwa ampenda kweli kweli,
Akaiba moyo wake kwa nadhiri za imani,
Isiyokuwa ya kweli.
LORENZO: Ni usiku kama huu,
Ndipo kizuri Jessika, kama kibibi mzozi,

Alimwamba kipenziye, naye akamwia radhi.
JESSIKA: Kama hangekuja mtu ningekupiku usiku,
Hebu lakini, sikia, kuna miguu ya mtu.
LORENZO: Nani aja kasi hivyo kwenye kimya cha usiku?
(*Stefano anaingia*)
STEFANO: Rafiki.
LORENZO: Rafiki, rafiki gani? Jina lako, tafadhali?
STEFANO: Jina langu Stefano; nakuletea habari,
Bibi mkubwa wa kwangu atafika Belimonti
Kabla jua kutoka: anatembeatembea
Mahali patakatifu anakopiga magoti,
Na kusali akiomba maisha mema ya ndoa.
LORENZO: Afuatana na nani?
STEFANO: Hafuatani na mtu,
Ila walii mpweke pamoja na mwali wake.
Nakusihi, tafadhali, bwanangu amesha rudi?
LORENZO: Hajarudi, na hatuna habari kutoka kwake.
Walakini nenda ndani, ninakusihi, Jessika.
Na tuanze kwa sherehe kuandalia tayari,
Angalau mapokezi ya Bibie mwenye nyumba.
(*Aingia Launseloti*)
LAUNSELOTI: Sola, sola! wo ha! So la!
LORENZO: Ni nani huyo aita?
LAUNSELOTI: Sola! Ulimwona Bwana Lorenzo? Bwana Lorenzo, sola, sola!
LORENZO: Acha ku-sola-sola, wee: hapa.
LAUNSELOTI: Sola! Wapi? Wapi?
LORENZO: Hapa.
LAUNSELOTI: Mwambie kuna mjumbe kutoka kwa bwana wangu ambaye kaja na baragumu lililojaa habari njema: bwana wangu atafika hapa kabla ya asubuhi.
(*Anatoka*)
LORENZO: Kipenzi, na twende ndani, tungojee kuja kwao.
Walakini haidhuru: kwa nini tuende ndani?

Mwenzi wangu Stefano, nakusihi tafadhali,
Kawajulishe wa ndani kuwa Bibi yako aja.
Halafu muziki wake utoe ulete nje. (*Anatoka*)
Jinsi gani mbaamwezi inavyolala unono,
Juu ya maua haya! Basi natuketi hapa,
Na sauti za muziki zitwingie sikioni:
Shwari tamu na usiku vyalaiki nyimbo tamu.
Kaa kitako, Jessika. Tazama namna mbingu
Ilivyopambwa kwa njumu za vipete vya dhahabu.
Kila nyota uonayo, japo ni ndogo ya zote,
Katika mwenendo wake hwimba kama malaika,
Kwa mlingano daima pamoja na Cherubimu
Wenye macho ya ujana: mlingano kama huo
U ndani ya roho zote za uzima wa milele;
Bali kama vazi hili la matope na kuoza
Lingali lauzingia hatuwezi kusikia.

(*Wanamuziki waingia*)

Njoni, haya, na kumwamsha Diana kwa muziki!
Kwa nyimbo bora za zote yapenyeni masikio
Ya mamenu na kumwita aje nyumbani kwa nyimbo.

(*Muziki*)

JESSIKA: Daima sichangamki nisikiapo muziki.
LORENZO: Sababu ni usikivu wa ndani ya moyo wako:
Litazame japo kundi la wanyama wa porini,
Au la wanafarasi ambao hawajafunzwa,
Wakirukaruka ovyo na kupiga makelele,
Ambayo ni kawaida ya hali ya damu yao;
Kwa bahati wasikie sauti ya tarumbeta,
Au muziki wo wote, iwaguse masikio,
Mara utaona wote wakisimama pamoja.
Na macho yao makali yameshikwa mshangao
Kwa uwezo wa muziki: hivyo basi, mshairi
Alitunga na kusema Orfeo wa zamani
'Liweza kuvuta miti, na mawe na mafuriko;

Kwani hapana cho chote kizito cha jinsi gani,
Au kigumu cha moyo, kilichojaa ghadhabu,
Kisoweza kugeuzwa na muziki kwa kitambo.
Mtu aso na muziki ndani ya nafsi yake,
Na wala hasisimki kwa utamu wa sauti,
Anafaa usaliti, ushabiki, na mateka.
Vitendo vya moyo wake sawa usiku wa giza,
Pia na mapenzi yake giza kama jehanamu.
Mtu wa namna hiyo hafai kuaminiwa.
Hebu, sikia muziki.

(*Aingia Poshia na Nerissa*)

POSHIA: Mwanga ule tuonao wawaka chumbani mwangu
Jinsi kishumaa kile kiangazavyo kwa mbali!
Ndivyo ling'aavyo jema katika dunia mbaya.

NERISSA: Mwezi ulipoking'aa hatukwona mshumaa.

POSHIA: Ndivyo utukufu bora hufifiliza hafifu:
Badala hung'aa sawa na mfalme mwenyewe
Kama mwenyewe hayupo; bali akisha kuwepo
Hujimimina hadhiye, kinavyofanya kijito,
Kunako wingi wa maji. Muziki! Hebu sikia!

NERISSA: Ni muziki wako, bibi, bendi yako ya nyumbani.

POSHIA: Naona hapana jema, bila mazingira yake:
Nadhani unapendeza kuuzidi wa mchana.

NERISSA: Shwari inaupatia uwezo huo, bibie.

POSHIA: Kunguru huimba vema kama kipozamatata
Ikiwa hasikilizwi; nafikiri kurumbiza
Angeliimba mchana, mabata wakitetea,
Hangedhaniwa mwimbaji kumzidi dudumizi.
Vitu vingi duniani hukolezwa na majira
Ndipo vikaifikia sifa yao hasa hasa,
Na kuwa vikamilifu. Kimya! Mwezi umelala,
Pamwe na Endimioni, hautaki kuamshwa.

(*Muziki unanyamaza*)

LORENZO: Ikiwa sikukosea asemaye ni Poshia.

POSHIA: Ananijua kipofu amjuavyo mlembe,
Kwa sauti yake mbaya.
LORENZO: Bibi, karibu nyumbani.
POSHIA: Tumekuwa tukisali kwa afya za bwana zetu,
Ambao twatumaini wanakuja kwa haraka
Kupita maneno yetu. Je, wamekwisha kurudi?
LORENZO: Hawajarudi, bibie, lakini kaja mjumbe,
Kusema wako njiani.
POSHIA: Enenda ndani, Nerissa; waamuru watumishi
Katu wasiseme kuwa tuliondoka nyumbani;
Na wala wewe, Lorenzo; na wewe pia, Jessika.
(*Sauti ya tarumbeta*)
LORENZO: Mumeo amesha fika; nasikia panda lake:
Sisi siyo sakubimbi, usihofu kitu, Bibi.
POSHIA: Usiku huu, nadhani, ni mchana taabani;
Unafifiafifia: walakini ni mchana,
Kama mchana ulivyo jua linapofichika,
(*Waingia Bassanio, Antonio Gratiano na Wafuasi wao*)
BASSANIO: Kama ungalitembea bila mwangaza wa jua.
Tungeupata mchana kwa wakati ule ule
Umulikapo dunia kule upande wa pili.
POSHIA: Nachie nitadhayali, bali nisiwe dhalili;
Maana mke dhalili, hufanya mume thakili,
Bali kwangu Bassanio, kamwe 'sije kuwa hivyo:
Ila Mola yaongoze! Karibu nyumbani, Bwana.
BASSANIO: Nakushukuru, Bibie. Mkaribishe mwenzangu:
Ndiye huyu mtu yule; huyu ndiye Antonio,
Ambaye kanifanyia fadhila zisopimika.
POSHIA: Yakupasa kila hali umshikilie sana,
Nasikia alishikwa sana kwa ajili yako.
ANTONIO: Siyo zaidi kuliko nilivyokwisha kulipwa.
POSHIA: Bwana, twakukaribisha, karibu nyumbani kwetu:
Lazima ionekane kwa namna nyinginezo,
Kwa hiyo naufupisha uungwana wa maneno.

GRATIANO: (*Kwa Nerissa*) Naapa kwa mwezi ule ya kuwa wanionea;
Hakika, nilimpayo muandishi wa hakimu:
Huyo ambaye anayo angafa kwangu si kitu,
Madhali, kipenzi changu, waumwa kiasi hiki.
POSHIA: Ugomvi, lo, mara hii! Hicho cha mno ni nini?
GRATIANO: Kiduara cha dhahabu, kipete hafifu sana,
Alichokuwa kanipa, ambacho maneno yake,
Kwa dunia yalikuwa kama choro za mjume
Kwenye kisu, yakisema, 'Nipende, usiniache'.
NERISSA: Wasema juu ya choro au juu ya thamani?
Uliapa mbele yangu nilipokupayo pete,
Ya kwamba utaivaa hadi saayo ya kufa,
Kwamba utazikwa nayo muwe wote kaburini:
Japo si sababu yangu, bali kwa viapo vyako
Ulipaswa uitunze, usifarakane nayo.
Muandishi wa hakimu! La, Mungu hakimu wangu,
Mwandishi uliyempa hataota ndevu kamwe
Katika kidevu chake.
GRATIANO: Ataota akiishi awe janadume zima.
NERISSA: Naam, kama mwanamke ataishi awe dume.
GRATIANO: Sikia, nakuapia kwa mkono wangu huu,
Niliimpa kijana, mvuli mdogo hivi,
Mbaya tena mfupi, asokuzidi kwa kimo,
Muandishi wa hakimu. Kijana mpayukaji,
Aliyenisihi sana nimpe iwe fidia:
Sikuwa na moyo kamwe wa kuweza kumnyima.
POSHIA: Lazima niseme kweli, ulikuwa na lawama,
Kutoa upesi hivyo chanza hiba cha mkeo;
Kitu ulichokivishwa kwa viapo kwenye chanda,
Kikakazwa kwa imani juu ya maungo yako.
Nami nilimpa pete, mwandani wangu mpenzi,
Na kumfanya aape, asachane nayo kamwe,
Na mwenyewe huyu hapa, nathubutu kumwapia,

Hangeweza kuitoa wala kuivua chanda,
Japo ni kwa mali yote ya dunia hii nzima.
Kwa hiyo, Gratiano, ukitaka kweli hasa,
Wampa jonzi mkeo, kwa sababu mbaya mno:
Mimi ningefikwa hayo, yangenitia wazimu.

BASSANIO: (*Kando*) Lo, heri nikijikata chanda changu cha kushoto,
Na kusema kilikatwa nilipokiitetea.

GRATIANO: Bwana wangu Bassanio alitoa pete yake
Kwa hakimu alomwomba, tena ambaye kwa kweli
Aliistahili pia. Halafu mwandishi wake,
Msaidia kwandika, naye akaomba yangu:
Na mwandishi wala Bwana hakukubali cho chote
Ila hizo pete mbili.

POSHIA: Pete gani, bwana wangu?
Natumai hukutoa ulopata toka kwangu.

BASSANIO: Ningeweza kuongeza wongo juu ya hatia
Ningesema kuwa siyo: bali waniona chanda,
Hiyo pete hakinayo; kwani imekwisha kwenda.

POSHIA: Wala hauna ukweli moyowo uso imani.
Naapa, sitakubali kuwa mke wako sini,
Mpaka niione pete.

NERISSA: Nami siwi mke wako
Hadi niione yangu.

BASSANIO: Mpenzi, ungemjua niliyempayo pete,
Ungelijua ni nani niliyempea pete,
Ungeweza kutambua nilichotolea pete,
Kuwa si kwa urahisi niliiachia pete,
Kwamba kingine cho chote hakutaka ila pete,
Ungepunguza makali ya ghadhabu na simanzi.

POSHIA: Kama wewe ungejua thamani ya ile pete,
Au nusu ya thamani yake alokupa pete,
Au utu wako wewe kwa kutunza ile pete,
Basi, usingeliweza kuachana nayo pete.

Kuna mwanamume gani mkaidi jinsi hiyo,
Kwamba kweli ungependa kuikatalia pete
Ukipinga kwa juhudi, angekuwa hana haya,
Azidi kung'ang'ania kitu ambacho ni hiba?
Nerissa kanifundisha nini hasa nisadiki:
Ningafa ni mwanamke alo nayo ile pete.

BASSANIO: La, naapa, kwa heshima na roho yangu, bibie,
Katu siyo mwanamke alo nayo ile pete,
Bali ni mwanasheria ambaye alikataa
Dukati elfu tatu nilizompa badala,
Akang'ang'ania pete; ambayo nilimnyima
Nikamwacha ende zake, amepagawa huzuni:
Ijapokuwa ni yeye aloyaponya maisha
Ya mwenzi wangu mpenzi. Ningesemaje, bibie?
Nilikuwa sina budi kutuma apelekewe;
Nilitingwa na aibu pamoja na uungwana;
Utu wangu ulizia kuchafuliwa na ghera
Ya kukosa shukurani. Nisamehe, bibi mwema;
Maana nakuapia, kwamba ungelikuwepo
Nadhani ungenisihi nikupeyo ile pete
Umpe mwanasheria mstahilifu huyo.

POSHIA: Asije wakili huyo karibu na nyumba yangu:
Kwa kuwa anacho kito ambacho nilikipenda,
Na ambacho uliapa kuwa utanitunzia,
Nitakuwa mkarimu, kamawe ulivyokuwa;
Na kushindwa kumhini cho chote nilicho nacho.
Wala siyo mwili wangu, wala kitanda cha bwana:
Kwani nitamtambua, hakika sinayo shaka.
Kamwe usilale nje. Nichunge vizuri sana,—
La, usiponichunga, ukinacha peke yangu,
Kweli kwa heshima yangu (ambayo bado ni yangu)
Tajikuta nina huyo daktari kitandani.

NERISSA: (*Kwa Gratiano*) Na mimi kwa mwandishi wake; kwa hiyo fikiri sana

Jinsi unavyoniacha bila kuniangalia.
ANTONIO: Maskini ndimi chanzo cha magomvi yote haya.
POSHIA: Bwana, usihuzunike; bado unakaribishwa.
BASSANIO: Poshia, niwie radhi, kosa hili la muhali,
Na hapa, mbele ya hawa marafiki zetu wengi,
Nakuapia, kwa hayo macho yako yang'aayo,
Nijionamo mwenyewe—
POSHIA: Sikia anavyosema!
Humo kwenye macho yangu ajiona mara mbili;
Mmoja kwa kila jicho; kiapo cha nyuso mbili
Si kiapo cha thamani.
BASSANIO: Tafadhali, nisikie:
Nisamehe kosa hili, nakuapia kwa moyo
Kwamba sitavunja tena kiapo cho chote kwako.
ANTONIO: Nilipata kudhamini mwili wangu kumfaa,
Na kama si yeye huyo mwenye pete ya mumeo,
Mambo yangekwenda kombo: najidhaminisha tena,
Moyo wangu uwe haka, kwamba bwana mume wako,
Kamwe hatavunja tena imani kwa makusudi.
POSHIA: Basi utamdhamini. Na sasa mpeyo hii;
Na mwambie aitunze kuzidi ile nyingine.
ANTONIO: Apa, Bwana Bassanio, kuitunza pete hii.
BASSANIO: Wallahi, ni ile ile niliyompa wakili!
POSHIA: Nimeipokea kwake: nisamehe, Bassanio.
NERISSA: Wewe pia nisamehe, Gratiano wangu mwema;
Kwani mvulana yule yule mbaya na mfupi,
Muandishi wa hakimu alinipa pete hii.
POSHIA: Wote mna mshangao; hii hapa ni barua,
Isomeni baadaye, mtapopata wasaa;
Inatokea Padua; yatoka kwa Bellario:
Humo mtaona kuwa Poshia ndiye wakili,
Na yule Nerissa pale ndiye muandishi wake,
Na Lorenzo huyu hapa atashuhudia kuwa
Nilitoka mara nyinyi mlipokwisha kutoka,

Na ndiyo mara nirudi; sijaingia nyumbani.
Antonio, karibu. Tena nina habari njema
Kuzidi matarajiyo: fungua barua hii.
Humo utakuta kuwa merikebu zako tatu
Zenye wingi wa shehena zi ghafla bandarini:
Hutaweza kufahamu namna nilivyoweza
Kupata barua hii.

ANTONIO: Nimepigwa bumbuazi.

BASSANIO: Mwanasheria ni wewe, nami nisikutambue?

GRATIANO: Wewe ndiwe muandishi?

ANTONIO: Bibi mwema, umenipa maisha na meshilio:
Kwani nasoma hakika kuwa kweli meli zangu
Zi salama bandarini.

POSHIA: Na wewe nawe Lorenzo!
Na kwako pia mwandishi wangu anazo faraja.

NERISSA: Naam, na nitampa bure bila ya fidia.
Pokeeni na Jessika kutoka kwa Myahudi,
Hati ma'lum ya hiba, baada ya kifo chake,
Ataacha kwenu nyinyi, kila atachokiacha.

LORENZO: Mabibi wema, mwanyesha manna kwa walo na njaa.

POSHIA: Kunakaribia kucha, lakini nina hakika
Bado hamjaridhika kabisa na mambo hayo.
Kwanza na twendeni ndani, kisha huko tuhojini
Nasi tutawajibuni mambo yote sawasawa.

GRATIANO: Haya basi, iwe hivyo.
Lo, maisha yangu yote hakuna kitu kabisa,
Ambacho nitakitunza kama pete ya Nerissa.

(*Wanatoka*)

Mabepari wa Venisi ni tafsiri ya kwanza ya Kiswahili ya ule mchezo wa kuigiza uitwao *The Merchant of Venice* uliotungwa na William Shakespeare. Kwa kuufasiri mchezo huu, baada ya *Juliasi Kaizari*, Mwalimu Julius K. Nyerere amewapatia nafasi watu wengi kusoma na kuigiza mmojawapo wa michezo ya kuigiza ya Shakespeare inayopendwa mno. Vile vile ile tafsiri yake ya *Julius Ceaser* sasa inapatikana kwa jina la *Juliasi Kaizari* ambayo yeye mwenyewe ameirudia na kuitengeneza zaidi.

OXFORD UNIVERSITY PRESS
EAST AND CENTRAL AFRICA

ISBN 0 19 572170 5